**KATAZO** la sigara hadharani, kutema mate barabarani
UKURASA 4



**RC** asema nguvu itatumika kumaliza mgomo daladala
UKURASA 4



UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Mei 15, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580581

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


# YALIYOTIKISA EID

**SAMIA** atilia mkazo mambo 10, Dk. Mwinyi ataka wananchi wajiandae Hijja Makka...*Endelea Ukurasa 2*





Waumini wa dini ya Kiislam wakishiriki swala ya Eid El Fitri, katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 5**

### WAZIRI AMPA MKURUGENZI SIKU SABA KUHUSU MACHINJIO

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amemwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora, Bosco Ndunguru, katika kipindi...

**UKURASA WA 5**

### WENYE LESENI BILA KUCHIMBAMADINI SASA KUPOKWA MAENEO

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, amemwagiza ofisa madini mkoa wa Njombe kuhakikisha anazichambua leseni zote 245...

# Wasia wa Mwinyi kwa Watanzania

UKURASA3

# PONDA ATAKA KATIBA MPYA

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA, KAIZER NI MTIFUANO** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Ujumbe kudumisha amani watawala

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa dini ya Kiislamu wamewataka waumini wa dini hiyo na Watanzania kwa ujumla kudumisha amani, kushirikiana katika masuala mbalimbali na kuepuka mifarakano isiyokuwa ya lazima.

Shekhe wa Mkoa wa Mwanza, Hassan Kabeke, alitoa rai hiyo wakati wa swala ya Eid iliyoswaliwa katika Viwanja vya Nyamagana.

"Katika hii dunia mitafaruku, migongano haiepukiki, hivyo sisi Waislamu yanapotokea haya tuwe wamoja na kuhakikisha yameisha na kujenga upendo mkubwa jambo ambalo Mungu atatufungulia baraka katika maisha yetu," alisema.

Aliwataka Waislamu na Watanzania kuhakikisha wanadumisha amani pamoja na kuiombea nchi na Rais Samia Suluhu Hassani pamoja na viongozi wengine.

Mkoani Dodoma, Shekhe wa Mkoa huo, Mustaph Rajabu, aliwataka waumini wa dini mbalimbali nchini kuendelea kulinda amani iliyopo nchini na kumuombea Rais Samia.

Akitoa mawaidha katika sala ya Sikukuu ya Eid kwa waumini wa Kiislamu kwenye Msikiti wa Gadaff jijini hapa, Shekhe huyo alisema suala la kuwaombea viongozi ni jukumu la kila Mtanzania, hivyo waendelee kuwaombea huku wakidumisha na kulinda amani.

"Kufungua kwa Ramadhani kusiwarudishe nyuma na kufanya matendo maovu, bali muongeze kasi zaidi ya kumwabudu Mungu," alisema.

Imamu Mkuu wa Msikiti wa Bilali Area 'C' jijini Dodoma, Hilal Abdul Azizi Yunus, akitoa hotuba katika suala ya Eid El Fitri iliyofanyika katika Uwanja vya Jamhuri, alisema Waislamu wanatakiwa kuwa kitu kimoja ili kuwa na nguvu moja kwa kuwa migogoro inasambaratisha na kuupunguzia nguvu Uislamu.

Mkoani Shinyanga, ujumbe uliotolewa jana uligusia kuwatiii na kuwaheshimu viongozi wa kiserikali akiwamo Rais Samia.

Shekhe wa Mkoa wa Shinyanga, Ismail Makusanya, Alisema maagizo ya kutii viongozi yanatoka kwa Mungu, hivyo ni vyema waumini hao wakafuata maagizo hayo na kuwatiii viongozi wa nchi na kuwaheshimu ili kujiongezea thawabu.

"Ninawaomba waumini wa dini ya Kiislamu tuwatii viongozi wetu wa serikali, uwe una wakubali ama kuwakataa, na hata kama huwapendi ama unawapenda, akiwamo Mkuu wetu wa Mkoa hapa Shinyanga, Zainab Telack na kiongozi wetu wa nchi, Rais Samia," alisema.

Shekh wa Wilaya ya Shinyanga, Soud Kategile, aliwataka Waislamu washikamane na kuwa wamoja kwa kila jambo, ili wafanikiwe katika mipango yao.

● **Imeandikwa na Paul Mabeja na Peter Mkwavila (DODOMA), Rose Jacob (MWANZA) na Marco Maduhu (SHINYANGA).**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitoa mkono wa Eid El Fitri kwa wananchi waliofika katika viwanja vya Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Samia atilia mkazo mambo 10 Eid

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesisitiza mkazo kuhusu masuala 10 wakati Waislamu wa Tanzania wakiungana na wenzao ulimwenguni kusherehekea sikukuu ya Eid el fitr jana.

Masuala hayo ni pamoja na usalama wa nchi, wananchi kuwa na matendo mema, janga la corona, wafanyabiashara kulipa kodi, watumishi kuepuka vitendo vya wizi na rushwa, haki, uhuru wa vyombo vya habari na demokrasia.

Akizungumza katika Baraza la Eid lililoandaliwa na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) mkoani Dar es Salaam, Rais Samia aliwahakikishia Watanzania serikali itakuwa imara kuhakikisha amani na usalama unaendelea.

Rais aliwataka Waislamu kuendeleza uchamungu walioonyesha wakati wa mfungo wa Ramadhani kwa kuwa na matendo mema ya kumpendeza Mungu na kufanya kazi kwa bidii na uadilifu.

"Ninawasihi watumishi wa serikali na sekta binafsi kuhakikisha wanafanya kazi na kupata kipato halali, wajiepushe na vitendo vya wizi, rushwa na ubadhirifu na urasimu.

"Kwa upande wa wafanyabiashara ninawahimiza kulipa kodi stahiki kwa serikali, siyo haki wala uungwana kukwepa kulipa kodi, kufanya hivyo kutaifanya serikali ishindwe kutoa huduma muhimu kwa wananchi," alisema.

Rais alisema wakifanya hivyo watasababisha hospitali kukosa dawa, watumishi kukosa mishahara na haki zao stahiki na wanafunzi watakosa elimu bure.

Alisisitiza umuhimu wa kila mmoja kuendelea kuishi kwa matendo mema waliyoishi wakati wa funga ya Ramadhani.

Pia, alitumia fursa hiyo kuwapongeza waumini wa dini zingine ambao kwa namna moja walishirikiana na Waislamu katika kipindi cha Ramadhani iwe kwa kufunga au kujizuia kufanya baadhi ya mambo ambayo yangewakwaza waliofunga.

Alisema pamoja na tofauti za dini, kabila, rangi na itikadi wamekuwa wakishirikiana kwenye masuala mbalimbali na kuwaeleza kuwa hawana budi kuendeleza utamaduni huo walioritishwa na waasisi wa taifa.

Kuhusu salamu za Baraza Kuu la Waislamu Tanzania zilizozungumzia amani, Rais Samia alisema serikali itakuwa imara katika kuhakikisha amani na usalama vinaendelea kudumu na kuwasihi wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa sababu jukumu la kuilinda ni lao wote.

Pia, alisema salamu za BAKWATA zilizungumzia kukuza uchumi na aliishukuru baraza hilo kuunga mkono serikali katika jitihada kukuza uchumi na hatua za kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara.

Alisema amefurahishwa na kitendo cha baraza hilo la kutaka kuanzisha miradi mbalimbali kwa ajili ya kukuza uwezo wa kiuchumi wa taasisi na mtu mmoja mmoja na kueleza hiyo inaendana na dhamira ya serikali ya kuhamamisha watu mbalimbali kuwekeza Tanzania ili kukuza uchumi, kupambana na umaskini na kuongeza ajira.

Rais Samia alihimiza taasisi zingine za dini nazo ziongeze jitihada kukuza uchumi wao na kuongeza mapato ili ziweze kumudu kuendesha vyema shughuli zao.

Akizungumzia salamu za BAKWATA zilizotolewa kuhusu malezi bora kwa vijana, uhuru, haki demokrasia, utawala bora na uhuru wa vyombo vya habari, Rais Samia alisema yote ni muhimu.

"Malezi bora kwa vijana ni muhimu siyo tu kuifanya jamii iondokane na vitendo viovu ukiwamo wizi, ujambazi, rushwa, ubadhirifu wa mali za umma, matumizi ya dawa za kulevya, yatawafanya vijana kushiriki katika shughuli za maendeleo na kutoa mchango stahiki kwenye familia, jamii na taifa," alisema.

Alisema serikali itaheshimu misingi ya haki uhuru na demokrasia na utawala bora kwa sababu masuala hayo ni muhimu katika kudumisha amani na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Kuhusu janga la corona, Rais alisema ili kukabiliana nalo hawana budi kushirikiana na wenzao duniani na kuwahakikishia tahadhari walizozitoa za chanjo zitafuatwa kikamilifu na serikali.

"Hii haina maana kwamba tutapokea kila kitu tunacholetewa au kuambiwa, la hasha! Ni lazima na sisi tujiridhishe, hata suala la chanjo tutajiridhisha kabla ya kuamua kutumia au kuacha kutumia, Watanzania wasiwe na hofu serikali ipo makini katika kushughulikia suala hili," alisema.

Katika hafla hiyo aliwashukuru viongozi wa dini kwa kuwa naye bega kwa bega tangu kuapishwa kwake na amefurahishwa na BAKWATA ambao wamemwahidi kutoa ushirikiano kwake na serikali kwa ujumla.

**SALAMU ZA BAKWATA**

Akisoma salamu hizo jana, Katibu Mkuu wa Baraza, Alhaj Nuhu Jabir Mruma, alisema baraza mara kwa mara limekuwa likiwasihi Waislamu kuendelea kuilea amani kama ilivyotunzwa na wazee waliotangulia mbele ya haki.

Kuhusu hotuba ya Rais Samia aliyoitoa Ijumaa iliyopita wakati akizungumza na wazee wa Mkoa wa Dar es Salaam ambayo iligusia mporomoko wa maadili, Alhaj Mruma alisema wana jukumu la kuwalea vijana.

Alisema BAKWATA pia imewataka Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari huku wakimpongeza Rais Samia kwa kuunda kamati ili kuishauri serikali namna bora ya kukabiliana na corona.

**MUFTI MKUU**

Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, aliwasisitiza Waislamu na Watanzania kwa ujumla wasipuuze hata kidogo suala la corona na kuwataka kufuata tahadhari zote zinazotakiwa kufanywa.

Alitoa nasaha kwa Waislamu na kuwaeleza kuwa anafahamu wamemaliza mwezi wa Ramadhani na kuwataka kufanya tathmini nini wamekivuna na faida waitumie miezi 11 waliyoianza jana.

Kadhalika, alimwomba Rais Samia kuangalia suala la tende ambazo hutumika wakati wa Ramadhani kwa kuwa wanaowaletea, hawana msamaha.

# Rais: Kaeni tayari kwa hijja Makka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewaongoza waumini wa dini ya Kiislamu katika ibada ya sala ya Eid elfitri katika Viwanja vya Maisa mjini Unguja na katika Baraza la Iddi lililofanyika Ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar.

Katika ibada hiyo viongozi mbalimbali wa kitaifa akiwamo Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla pamoja na marais wastaafu akiwamo Amani Abeid Karume na Makamu wa Rais mstaafu, Dk. Mohamed Gharib Bilali, walishiriki.

Akizungumza katika Baraza la Iddi, Rais Mwinyi aliwataka Waislamu kujitayarisha mapema kwa ibada ya Hijja kule Makka huku serikali ikisubiri maelekezo ya utaratibu wa kufanyika kwa ibada hiyo kutoka kwa mamlaka ya Sauda Arabia kufuatia janga la corona.

Alisema Serikali ya Sauda Arabia imetoa taarifa za awali za kufanyika kwa ibada ya Hijja kwa sharti la mahujaji kupata chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Rais Mwinyi alisema serikali itaweka taratibu na masharti ya kufikia vigezo vitakavyotolewa na mamlaka ya Serikali ya Sauda Arabia kwa ajili ya waumini wa dini ya Kiislamu kufanya ibada ya hijja ambayo ni miongoni mwa nguzo tano za dini ya Kiislamu ambayo hutekelezwa kwa mwenye uwezo.

"Ninapenda kuwajulisha ndugu Waislamu wenye nia ya kufanya ibada ya hijja huko Makka kwamba tunasubiri maelekezo na mwongozo wa kufanyika kwa ibada hiyo kutoka Sauda Arabia kufuatia kuwapo kwa ugonjwa wa corona ambapo wahusika wameweka masharti ya kupata chanjo kwa mahujaji," alisema.

Dk. Mwinyi aliuagiza uongozi wa kamisheni ya wakfu na mali ya amana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukamilisha mapendekezo ya kuanzishwa kwa mfuko wa hijja ambao utatoa nafasi kwa Waislamu wengi wenye nia ya kufanya ibada hiyo kutekeleza dhamira zao.

Alisema mfuko huo ni muhimu na malengo yake ni kutoa nafasi kwa waumini ya dini ya Kiislamu kutekeleza ibada hiyo kwa wale ambao hawana uwezo wa kifedha.

Alisema mfuko wa aina hiyo upo katika baadhi ya nchi zenye wafuasi wengi wa dini hiyo na umewawezesha wananchi wengi ikiwamo wasiokuwa na uwezo kutekeleza ibada hiyo. "Ninauagiza uongozi wa kamisheni ya wakfu na mali ya amana kukamilisha mapendekezo ya kuanzishwa kwa mfuko wa hijja ambao huo utawasaidia watu wasiokuwa na uwezo kutekeleza ibada hiyo," aliagiza.

Dk. Mwinyi aliwakumbusha Waislamu kuendelea kuzingatia mafunzo mazuri ya viongozi wa dini ikiwamo mashehe katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani ambacho kimejenga mshikamano na mapenzi na kuoneana huruma kwa kusaidiana.

Alipongeza uvumilivu wa kidini kwa wananchi wa Zanzibar ikiwamo watu ambao siyo Waislamu kwa kuheshimu mwezi mtukufu na kujizuia kufanya vitendo vyenye kukera na maudhi kwa watu wengine.

Alisema uvumilivu huo umeifanya Zanzibar kuwa miongoni mwa nchi zenye kuheshimu imani ya kidini kwa watu wengine tangu miaka ya tawala mbalimbali za kikoloni.

Katibu wa Mufti Zanzibar, Sheikh Khalid Mfaume, alimpongeza Rais Mwinyi kwa kuonyesha mfano wa kiongozi aliyefanya kazi kubwa ya kuwaunganisha Waislamu na kurudisha uelewano kwa watu waliokuwa na jazba na hasira za chuki za moyoni.

Aliyataja maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa yameondosha siasa za chuki na uhasama na sasa wananchi kuunganisha nguvu na umoja kwa ajili ya kujenga Zanzibar yenye neema nyingi.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akizuru kaburi la aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, aliposimama kwa muda wilayani Chato, akiwa njiani akielekea wilayani Kibondo, mkoani Kigoma jana, kwa ajili ya kufunga kampeni za ichaguzi mdogo wa ubunge za CCM za Jimbo la Muhambwe, unaotarajiwa kufanyika kesho. **PICHA: OMR**

# Wasia wa Mwinyi kwa Watanzania

**Na Sanula Athanas**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, ametahadharisha kuwa alichokiita hatari kubwa inayoweza kuingia nchini ikiwa Watanzania wakifanya kosa la kuendekeza ubaguzi kwa misingi ya dini au kabila za watu.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anatoa wasia wake kwa taifa, akisema Watanzania wanapaswa daima kumuenzi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kwa vita vyake vya dhati dhidi ya udini na ukabila.

Anasema Mwalimu alikuwa Mkristo, kutoka Tanzania Bara, tena Mkoa wa Mara, lakini akawa Dar es Salaam, akawaunganisha Waislamu na Wakristo, watu wa Bara na Pwani, kudai na hatimaye kupata uhuru.

"Kwa wale wanaoendekeza udini na ukabila watashangaa, Mwalimu Nyerere alichaguliwa na wazee wa Kiislamu kuwa Rais wa TAA na hatimaye TANU. Alilipa fadhila hiyo kwa kupiga vita udini na ukabila maisha yake yote ya uongozi wa siasa na serikali," anasema. Mwinyi anapongeza viongozi wakuu wa serikali kwa kuendelea kupiga vita udini na ukabila, akisihi:

"Ushauri wangu wa dhati kwa vizazi vya leo na vijavyo vya Watanzania ni kuwa tusije kulala usingizi. Ni rahisi sana kubomoa kuliko kujenga. Na kilichobomolewa kuja kukijenga upya ni kazi ngumu zaidi kuliko ilivyokuwa wakati kinajengwa mara kwanza.

"Angalia kwa mfano taabu inayotupata na muda mrefu unaochukuliwa kuijenga upya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo ndugu zangu Watanzania tusisinzie, wala kulala kuhusu vita dhidi ya ukabila na udini."Mwinyi anakumbusha kuwa mmojawapo ya watu waliokuwa mwiba kwake ni marehemu Mchungaji Christopher Mtikila, akidai ni kati ya watu waliokuwa na chuki dhidi ya Waislamu.

"Nilipomteua Mwislamu, Prof. Kighoma Malima kwa Waziri wa Elimu, ambaye alikuwa Waziri wa Elimu wa Muislamu wa kwanza, Mtikila alinishambulia sana, kwa lugha isiyostahili kabisa mtu anayesema ni kiongozi wa dini.

"Ni kweli walikuwapo pia baadhi ya maaskofu waliopata wasiwasi kuona nimemteua Mwislamu kuwa Waziri wa Elimu, lakini Mtikila alikuwa katika ligi ya peke yake.

"Kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM wa Oktoba 1987, Mtikila alimwandikia Mwenyekiti wa CCM, Mwalimu Nyerere, barua akinishambulia sana mimi na serikali yangu kuwa tunawaonea na kuwakwamisha Wakristo, jambo ambalo dhahiri lilikuwa la uongo na uzandiki usio na msingi wowote.

"Mimi nilishambuliwa pia na Waislamu wenzangu kuwa bado ninaendelea kupendelea Wakristo na kutotumia urais wangu kurekebisha kile wao walichokiona kama historia ya upendeleo wa Wakristo, jambo ambalo halikuwa na ukweli wowote. "Kwa maneno yake (Mtikila), ikaonekana kama ananituhumu kuwa ninatumiwa na Kiongozi wa Iran, Ayatollah Khomeini, kueneza ajenda ya Uislamu nchini.

"Ninatoa mfano huu mjue kwamba wakati mwingine inahitaji mtu mmoja wa ovyo hivi au mchonganishi mwenye mdomo mkubwa, akazua balaa kubwa kwenye eneo hili.

"Ninarudia. Watanzania, viongozi na wananchi, msije katu mkafumbia macho mbegu zozote, hata ziwe ndogo kiasi gani, za ukabila na udini. Majuto ni mjukuu," Mwinyi anasihi.

# Kina Ponda wamshauri Samia serikali shirikishi, katiba mpya

**Na Romana Mallya**

JUMUIYA na Taasisi za Kiislamu Tanzania, imeunga mkono tamko la Rais Samia Suluhu Hassan, la kuunda Serikali shirikishi, huku ikishauri kabla ya uteuzi huo wazungumze na vyama husika vya siasa ili kufikia makubaliano.

Ushauri wa jumuiya hiyo kwa Rais Samia umo katika waraka wake wa sikukuu ya Iddi El Fitri,

Tamko hilo ambalo lilisomwa jana na Katibu wa Jumuiya hiyo, Sheikh Issa Ponda, lilisema wanamuunga mkono Rais Samia kwa sababu wanaamini maendeleo huletwa kwa ushirikiano.

Mei 7, mwaka huu, Rais Samia, wakati akizungumza na wazee wa mkoa wa Dar es Salaam, aliahidi katika kupanga safu ya kujenga uchumi wa nchi, huko mbeleni bila kujali chama, atamteua Mtanzania yeyote mwenye weledi, umahiri, anayeweza kuleta manufaa kwa taifa kwa kutumia uwezo alionao. Katika tamko la Jumuiya na taasisi za kiislamu, Sheikh Ponda alisema wanamuomba Rais uteuzi huo wa viongozi uzingatie maadili, ujuzi na uwajibikaji.

Alisema kila Mtanzania ana haki ya kulitumikia taifa lake bila ya kubaguliwa kwa sababu ya siasa, kabila, jinsia au dini.

Pia wameshauri katika nafasi za kisera kama vile uwaziri, ukuu wa Mkoa na nyingine, anapotaka kumteua mtu wa chama cha upinzania katika nafasi hizo, ni vema afanye mazungumzo na chama husika ili wafikie makubaliano mazuri.

"Hatua hii itasaidia kuvilinda vyama vya upinzani visipoteze viongozi wao muhimu kwa kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na hatimaye kulirudisha taifa katika mfumo wa chama kimoja," jumuiya hiyo ilishauri.

Pia wameshauri Serikali ijipange kuamsha mchakato wa Katiba mpya ambao ulisitishwa ukiwa katika hatua za mwishoni.

"Katika kipindi hiki cha mpito, Serikali ianzishe mchakato wa kuundwa baadhi ya vyombo muhimu kama vile Tume Huru ya Uchaguzi Tanzania. Hii itaboresha mfumo wa siasa kwa uchaguzi utakaofanyika kabla ya Katiba Mpya kuwa huru na za haki," alisema.

Sheikh Ponda alisema Jumuiya na Taasisi za kiislam zinawakumbusha Waislamu umuhimu wa huruma na kujitakasa na maovu.

Alisema zinawataka Waislamu wajikite katika mambo ya kijamii kama kuanzisha vikoba kwa ajili ya ada za masomo kwa ndugu walio maskini na waimarishe programu za kuwasaidia wenye ulemavu, wagonjwa hospitalini na wafungwa magerezani. Alisema Ramadhani ina mafundisho mengi ya kiroho na ya kijamii na kwamba aliyefunga swaumu anapopata taarifa ya jamii iliyokumbwa na njaa au ukosefu wa maji, ni rahisi kwake kuelewa ukubwa wa tatizo.

## Fursa yaja soko la mahindi Kenya

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amewataka wakulima na wafanyabiashara wa mahindi kutumia fursa ya soko la Kenya, ikiwa sehemu ya ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuuza mazao yao.

Lengo la hati hiyo ni kujiingizia kipato na kuiletea nchi fedha za kigeni.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano wa wadau wa zao la muhogo ambapo pia alizindua mkakati wa zao hilo,

Prof. Mkenda alisema Wizara yake imejipanga vyema kuhakikisha tija ya uzalishaji inaongezeka na masoko yanapatika ikiwamo soko la mahindi nchini Kenya.

"Hivi karibuni wakuu wa Tanzania na Kenya walikutana na kujadiliana juu ya changamoto za ufanyaji biashara kati ya nchi hizo, hivyo mipaka imefunguliwa kwa wafanyabiashara kuendelea na shughuli zao kwa faida ya wote," alisema Prof. Mkenda.

Aliongezea kuwa ziara ya hivi karibuni ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Kenya imeleta mafanikio makubwa kwa wakulima na wafanyabiashara kwa kupata fursa ya kuingia na kuunga mazao yao Kenya.

"Katika kuhakikisha mambo yanakwenda vyema katika mipaka yetu, nimezungumza na Waziri wa Biashara na Kilimo nchini humo, Peter Munya, ambaye yupo njiani kuelekea Namanga katika kutekeleza maagizo ya viongozi wetu wakuu kuhakikisha biashara zinaendelea," alieleza.

Waziri Mkenda alisisitiza kuwa mazao ya Tanzania hususani mahindi na bidhaa nyingine ni salama, kwani kabla bidhaa haijasafirishwa nje ya nchi, mamlaka husika kama Shirika la Viwango (TBS), hufanya vipimo kuhakikisha viwango vinavyohitajika sokoni vimekidhi.




Wanafunzi wakisubiri usafiri katika kituo cha daladala cha Kimara Mwisho, Barabara ya Morogoro, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Baadhi ya makondakta na madereva wamekuwa wakiwaacha vituoni na kusababisha wachelewe kufika shuleni au nyumbani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Katazo sigara hadharani, kutema mate barabarani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ametolea ufafanuzi tena sakata la wabunge 19 wa Viti Maalum, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), akisema hawezi kuwafukuza hadi apate nakala za vikao vya chama hicho vilivyowafukuza uanachama.

Alitoa kauli hiyo bungeni jana akisisitiza kauli yake aliyoitoa mwanzoni mwa wiki kutokana na kuwapo kwa shinikizo la kuwafukuza wabunge hao bungeni.

Akizungumza jana baada ya kipindi cha maswali na majibu, Ndugai alisema ili atoe uamuzi kwa chama chochote cha siasa chenye nia ya kufukuza wabunge, ni lazima ajiridhishe kwa viambatanisho ambavyo ni katiba na muhtasari wa kuwafukuza kutoka kwenye chama husika.

"Nilitoa rulling (uamuzi) hapa ninaomba sasa nirudie tena maana wengine wanafikiri spika akiongea hapa ni masihara, spika anaongoza Bunge kwa kufuata kanuni, katiba sheria, utaratibu, utamaduni na uamuzi wa maspika wengine. "Uamuzi ninaotoa hapa ni uamuzi utakaotumika na hata watakaofuata baada yangu, rulling niliyotoa ninairudia, maana watu wanaweza kusema Ndugai hasa ni nani, suala siyo Ndugai, suala ni spika. "Ninarudia tena ili wanielewe vizuri maana hivyo ndivyo itakavyokuwa, hatulumbani, hapa sipo kwa sababu ya kulumbana na hii itatumika sasa na hata siku zijazo.

"Kwa vyama vyovyote vyenye kufukuza wabunge ambao ni wanachama wao, kwa kutumia dirisha la wanachama wao wanawafukuza watu ambao hao wanaofukuzwa ni wabunge," alisema.

Ndugai alisema wanapaswa wanapomwandikia Spika ni busara kumnakili Msajili wa Vyama vya Siasa.

"Lakini hata asipopeleka kule ni busara kufanya hivyo lazima barua hiyo iambatane na katiba yao, na muhtasari wa vikao vilivyohusika kuwafukuza wabunge hao," alisema. Spika Ndugai alisema kama vyama vitafanya hivyo, vitamrahisishia kazi yake katika kutenda haki ili kuona kama ni kweli haki imetendeka kabla ya yeye kuweka baraka zake ili asionee watu kwa sababu ambazo hazina mbele wala nyuma.

"Sasa kama sina hivyo viambatanisho hivi, nitajuaje? Hiyo kamati kuu ndiyo kamati kuu ya chama fulani, anayejua ni Msajili sasa lazima nipate nakala zile niweze kuona ili niwaite na hao wabunge husika.

"Niwaambie jamani ninayo maandishi hapa yanayosema kuna hiki na hiki na hiki mnasemaje ili nao wajitetee mbele yangu niweze kutoa uamuzi, vinginevyo haiwezekani tu kwa sababu fulani anataka jambo fulani halafu ikawa, haiendi hivyo ni masuala ya haki." Alieleza masuala ya haki yanataka utaratibu na kwamba hilo litatumika kwa yeye na maspika wanaofuata hivyo viongozi wa vyama wanaoandika barua ya aina hiyo waambatanishe vitu hivyo na kwakuwa katiba hizi zinabadilika badilika aletewe katiba ambayo ndio inafanya kazi wakati huo.

"Kwa hiyo wale wenye nia hizo mnaogopa nini kuambatanisha hizo nakala za vikao vyenu? Kwa nini mnafichaficha, kuna nini ndani yake? Mbona ni jambo rahisi tu, mnaniletea mimi ninafanya kazi yangu wala haina shida," alisema.

# RC: Tutatumia nguvu mgomo wa daladala

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameahidi kumaliza mgomo wa daladala uliodumu kwa siku nne mfululizo jijini Mbeya akisisitiza atalazimika kutumia nguvu kwa kuwa anaamini mgomo huo umetokana na kiburi cha madereva wa daladala.

Alitoa kauli hiyo jana alipohutubia kwenye Ibada ya Sikukuu ya Eid El Fitr iliyofanyika kimkoa katika Uwanja wa Kumbukumbuku ya Sokoine jijini Mbeya.

Chalamila alisema walikuwa wanashindwa kutumia nguvu kwenye utatuzi wa mgogoro uliopo kutokana na baadhi ya watu kuwa kwenye mfungo wa Ramadhani na hivyo waliamua kutumia njia za kidiplomasia kutatua.

Alisema hawezi kukubali wananchi waendelee kupata shida ya usafiri kwa sababu ya watu wachache ambao wameamua kugoma na kwamba huo mgomo utafika mwisho na wananchi wataanza kutumia usafiri wanaoutaka.

"Migogoro huwa tunaanza kuitatua kwa mazungumzo lakini kama mazungumzo hayo hayafikii mwisho na ndani yake kukiwa na kiburi ujue kwamba sisi kama serikali hatutakubali wananchi waendelee kupata shida," alisema.

Chalamila alisema wamiliki wote wa vyombo vya usafiri katika mkoa huo wanatoa huduma ya aina moja, hivyo wanatakiwa waheshimiane kulingana na kila mmoja chombo anachomiliki na riziki anayopata.

Alisema wamiliki wa daladala wanatakiwa kuheshimiana na wamiliki wa vyombo vingine wakiwamo wamiliki wa bajaj na pikipiki za kubeba abiria, maarufu bodaboda.

Alisema endapo wamiliki wa daladala watafumbiwa macho wakaendelea na manyanyaso dhidi ya wamiliki wa vyombo vingine vya usafiri, kuna uwezekano migogoro ya aina hiyo ikaendelea.

"Itafika kipindi wenye malori makubwa watataka malori madogo yatoke barabarani, wenye mafuso makubwa watataka wenye mafuso madogo waondoke barabarani, sasa hatuwezi kufikia huko," alionya.

Chalamila alisema Jiji la Mbeya lina tatizo la miundombinu ya barabara, hivyo uongozi wa mkoa unaendelea na mazungumzo na Rais ili mkoa huo uongezwe bajeti ya ujenzi wa barabara.

Alisema endapo barabara hizo zitakamilika ndipo watakuja na utaratibu wa kupanga vizuri vyombo vya usafiri ikiwamo kutenga barabara za daladala, za bajaji na za watembea kwa miguu.

Juzi, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema hawana mpango wa kuziondoa bajaj barabarani kama wanavyotaka madereva daladala.

Alisema katika jiji hilo kuna bajaji zaidi ya 3,000 ambazo zimeajiri idadi kubwa ya vijana na hivyo kuziondoa bajaji hizo ni kuharibu ajira za kundi kubwa la vijana.

Hata hivyo, alisema tatizo lililopo ni kwamba sio madereva daladala wote wanaukubali mgomo huo isipokuwa wanashinikizwa na wenzao wachache.

Mgomo huo wa daladala ulianza Mei 11 mwaka huu ambapo madereva daladala wanaishinikiza serikali kutekeleza maazimio 10 ambayo walikubaliana Machi mwaka huu likiwamo la kuziondoa bajaj kwenye barabara zilizotengwa kwa ajili yao.



Vijana wakijitolea kutengeneza barabara ili watu wapite kwa urahisi katika Mto Tegeta, eneo la Goba jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wenye leseni bila kuchimba madini sasa kupokwa maeneo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, amemwagiza ofisa madini mkoa wa Njombe kuhakikisha anazichambua leseni zote 245 za wachimbaji mkoani hapo, ili kuwapata wenye maeneo makubwa yasiyo endelezwa.

Imeelezwa kuwa baada ya hapo yatakabidhiwa kwa wachimbaji wadogo wenye uwezo wa kuyaendeleza.

Pia, ameutaja Mkoa wa Njombe kukusanya kiwango kidogo cha mapato, kulinganisha na malengo ambayo yamewekwa kwenye sekta hiyo, ambapo umekusanya kiasi cha Sh. milioni 240 pekee kati ya Sh. bilioni moja, ambayo ilitarajiwa kukusanywa.

Alitoa agizo hilo wakati akizungumza na wachimbaji wadogo wa madini Mkoa wa Njombe, ambapo alisema mkoa huo una takribani leseni za wachimbaji madini 245, lakini wengi wao hawazifanyii kazi wakati kuna wachimbaji wengine wana mitaji, lakini wanakosa leseni.

"Kama watu wameshikilia maeneo makubwa na hawawezi kuchimba, inawabidi kumega ili kuwapatia wachimbaji wadogo, kwani serikali inatoa leseni ili ziweze kutumika na siyo kukaa kabatini," alisema.

Alisema: "Tunategemea Mkoa wa Njombe uwe na makusanyo makubwa, kwa sababu kuna makaa ya mawe, chuma na mengine, lakini hakuna uchimbaji kwa sababu tu watu wameshikilia leseni na hawazifanyii kazi miaka nenda rudi."

Prof. Msanjila aliongeza: "Tunalifanyia kazi tuone ni namna gani na wachimbaji wadogo wanaweza kupata hizo chache na wameomba chache. "Wataalamu watuambie wanapendekeza nini juu ya hizo leseni... nafikiri humo ndiyo tutapata hizo mnazoziomba."

Mmoja wa wachimbaji wadogo, Salum Sanga, alilalamikia wachimbaji wakubwa kwa kuhodhi maeneo makubwa, ambayo hawayafanyii kazi likiwamo Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC).

Naye Mwenyekiti wa wachimbaji wadogo wa madini mkoani Niombe, Alfred Luvanda, alisema kuna zaidi ya wachimbaji wadogo 200 katika mkoa, ambao baadhi yao wamekuwa na mitaji, lakini wanakosa leseni, na kwamba wataishukuru sana wizara ikitekeleza maombi yao.

# Machinjio Tabora yamkera waziri Jafo

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amemwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora, Bosco Ndunguru, katika kipindi cha siku saba kuhakikisha machinjio katika Manispaa yake yanafanyiwa usafi madhubuti.

Alitoa agizo hilo juzi katika ziara yake ya kikazi ya kukagua usimamizi na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 mkoani Tabora. Akiwa katika machinjio hayo, Waziri Jafo alishuhudia kukithiri kwa uchafu ndani na nje ya jengo hilo, jambo ambalo linahatarisha afya za wakazi wa Tabora.

"Mazingira ya hapa ni machafu sana, ninatoa muda wa wiki moja marekebisho yafanyike na nipate taarifa ya utekelezaji mapema iwezekanavyo pia ninatoa mwezi mmoja wa ukarabati wa mfereji wa maji taka," Jafo aliagiza.

Waziri huyo alitembea kampuni ya kuzalisha mkaa mbadala ya 'Kuja na Kushoka' na kutoa rai kwa taasisi za umma na binafsi kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuhamasisha matumizi ya mkaa mbadala unaozalishwa kutokana na taka.

"Azma ya serikali ni kuhakikisha tunatunza mazingira yetu kwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, ninatoa rai kwa shule za binafsi na za serikali kununua hizi mashine za kuzalisha mkaa badala ili zitumike kuzalisha mkaa katika shule zao pia kama chanzo cha mapato kwa kutengeza mkaa na kuuzia wengine," aliagiza.

Akiwasilisha taarifa ya kampuni ya kuzalisha mkaa mbadala, Leonard Kushoka, alisema anatumia teknolojia ya kuchakata taka na kuzalisha mkaa mbadala ambao umekuwa wa manufaa kwa wakazi wa Tabora na Tanzania kwa ujumla kwa kutoa ajira kwa vijana na kunusuru mazingira.

Waziri Jafo alikuwa mkoani Tabora kukagua shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira ambapo kwa siku ya kwanza alikagua Machinjio ya Manispaa ya Tabora, Kampuni ya Kuzalisha Mkaa Mbadala na ukaguzi wa mabwawa ya maji taka.

# PBZ yakumbuka yatima Mtwara

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

BENKI ya Watu wa Zanzibar (PBZ) mkoani Mtwara, imekabidhi msaada wa shehena ya vyakula mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 9 kwa watoto yatima waishio katika Manispaa ya Mtwara.

Msaada huo ulitolewa jana mkoani Mtwara katika Kata ya Jangwani, Mtaa wa Mtangashari, Manipsaa ya Mtwara Mikindani na kupokelewa na watoto hao pamoja na serikali ya mtaa.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, afisa masoko wa Benki hiyo, Nassoro Mohamedi, alisema msaada huo ni mwendelezo wa kusaidia makundi maalumu katika jamii kwa kutoa mahitaji mbalimbali hasa katika kipindi hiki cha sikukuu ya Eid el ilivyo kwa makundi mengine.

Alisema katika sherehekea sikukuu hiyo, kila mmoja anapaswa kuwa na furaha, hivyo makundi maalumu pia wana haki ya kusherehekea, na kwamba ni bora na wao wakapata chakula na mahitaji mengine ya msingi.

Mohamedi alisema Benki ya Watu wa Zanzibar imeamua kufika katika Manispaa ya Mtwara Mikindani kwa watoto hao yatima na kuwapatia msaada huo wa vyakula viweze kuwasaidia wakati wa sikukuu.

Alisema msaada huo unajumuisha ngano, mchele, mafuta ya kula, unga wa sembe na maharagwe, na kwamba vyakula hivyo vilivyotolewa kwa watoto hao yatima vitaweza kwenda kuwasaidia nyumbani kwao wakiwa na familia zao.

Nassoro alisema jumla ya watoto 76 waliopo katika Mkoa wa Mtwara wamefikiwa na PBZ kwa kupatiwa msaada wa mahitaji mbalimbali vikiwamo vyakula.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Salama Salumu, mtoto yatima aliishukuru kitendo cha kuwatafuta na kuwapatia vyakula kwa ajili ya sikukuu ya Eid el Eid, na kwamba wao wamejisikia fuhara.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba malizieni kazi robo fainali CAF ugenini leo

**MIAMBA** ya Ligi Kuu Tanzania Bara, leo itashuka katika Uwanja wa FNB maarufu Soccer City ama 'The Calabash', ugenini Afrika Kusini kuivaa Kaizer Chiefs katika mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika mchezo huo utakaopigwa majira ya saa 12:00 jioni kwa Afrika Kusini sawa na saa 1:00 usiku Afrika Mashariki, timu zote zitakuwa zikihitaji ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele hatua ya nusu fainali zitakaporudiana hapa nchini Jumamosi ijayo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Simba inapewa nafasi kubwa ya kusonga mbele kutokana na rekodi yake nzuri kwenye michuano hiyo msimu huu baada ya kuongoza kwenye msimamo wa Kundi A lililokuwa likijumuisha mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Ahly ya Misri, timu ngumu na zoefu ya AS Vita ya DR Congo na vigogo Al-Merrikh ya Sudan.

Katika hatua hiyo, Simba ilimaliza ikiwa na pointi 13 baada ya kushinda mechi nne, sare moja na kupoteza mchezo mmoja ugenini dhidi ya Al Ahly ikiwa ni baada ya kuwanyuka mabingwa hao watetezi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa huku ikipata matokeo nyumbani na ugenini dhidi ya AS Vita na kisha kuichapa Al-Merrikh hapa nchini.

Lakini Kaizer Chiefs iliyokuwa Kundi C, ilimaliza nafasi ya pili kwa faida ya 'head to head' (matokeo ilipokutana) na Horoya FC ya Guinea baada ya timu hizo kila moja kumaliza na pointi tisa kutokana na kushinda mechi mbili, sare tatu na kupoteza mchezo mmoja, huku Wydad Casablanca ya Morocco ikimaliza kinara na Petro de Luanda ya Angola ikiburuza mkia.

Kinachowafanya wachambuzi na wadau wengi wa soka kuipa Simba nafasi ya kusonga mbele, si tu kutokana na takwimu hizo, bali pia kiwango cha juu ambacho kimekuwa kikionyeshwa na timu nzima na mchezaji mmoja mmoja tangu kuanza kwa michuano hiyo msimu huu.

Lakini pia ni uwezo mkubwa wa benchi la ufundi la kuwasoma wapinzani na mbinu zao mbadala likiongozwa na Kocha Mkuu, Mfaransa Didier Gomes, ambaye amekuwa kipenzi kikubwa cha mashabiki wa timu hiyo tangu arithi mikoba ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck aliyeiwezesha timu hiyo kufuzu hatua ya makundi na kutimka.

Pamoja na maoni mengi yaliyotolewa na yanayoendelea kutolewa na wachambuzi na wabobezi hao wa soka, bado Nipashe tunaamini hii ni hatua ngumu zaidi ambayo Simba inapaswa kuwa makini katika kila mchezo ili kuweza kusonga mbele.

Tunasema hivyo, kutokana na ukweli kwamba katika hatua hii matokeo huamuliwa zaidi na idadi ya mabao na hapa si suala la pointi, kwani ukipoteza ugenini ama nyumbani ukapata ushindi hafifu, tayari unaaga mashindano, hivyo ni mechi ambayo kila mchezaji anatakiwa kubeba zaidi ya jukumu moja uwanjani kwa kucheza kitimu.

Tunaamini Gomes na wasaidizi wake wana uzoefu mkubwa sana kimbinu kwa kuwasoma wapinzani, lakini kama ilivyo kwa Simba kupenda kumiliki mpira, ndivyo ilivyo kwa Kaizer Chiefs, ila timu hiyo ya Afrika Kusini yenyewe ina sifa kubwa ya kuwa na kasi inapokuwa na mpira, hivyo kamwe hauwezi kuwa mchezo rahisi kwa wawakilishi hao wa Tanzania kwenye michuano hiyo ya CAF.


Licha ya kutambua kwamba itakuwa mechi ngumu kwa kila upande, kinachotakiwa kwa Simba ni kuhakikisha inapata matokeo chanya ugenini na ikiwezekana kumalizia mechi hiyo huko huko Afrika Kusini kwa kupata ushindi wa kishindo ili kujirahisishia kazi katika mchezo wa marudiano wiki ijayo.

Nipashe kama ilivyo kwa Watanzania wote wenye mapenzi mema na soka la nchi hii, tunatamani kuona Simba ikipata ushindi wa kishindo leo ili kuendelea kusafisha njia kwa Tanzania kupata nafasi ya kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), hivyo tuna kila sababu ya kuitakia kila la kheri ya kupata matokeo chanya ugenini leo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Chuki humchoma anayeihifadhi

**KWA** kawaida chuki humsumbua anayeiweka au kuifadhili hiyo. Twafunzwa umuhimu wa kutoiweka chuki kwani tunajidhuru wenyewe.

"Utani" ni taratibu au desturi za kimila zinazowafanya watu wanaojuana waweze kuambiana au kutendeana jambo lolote la mzaha bila ya kuleta chuki au kero, maneno ya masihara, dhihaka.

Pia ni maneno au vitendo vya dhihaka; mzaha. Tabia ya watu kufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana kweli na kuimarisha uhusiano wao. Mzaha ni kauli ya utani; stihizai, michezo au masihara anayofanyiwa mtu; goya; dhihaka.

Leo usiku Simba itapambana na timu ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini na zitarudiana Mei 22 jijini Dar es Salaam ili kupata mshindi halisi atakayeendelea ilhali atakayeshindwa atajiuma vidole na kusonya kwa kubana mdomo wa chini na meno ya juu na kisha kutoa sauti nyembamba kuonesha dharau, chuki au hasira.

Simba na Yanga zachukiana mithili ya ashaakum kama m-mbwa na paka. Ashaakum ni tamko la kuomba radhi kabla ya kusema neno la karaha. "Chuki" ni hali ya kutokuwapo upendo; hali ya kuwa na roho mbaya, hali ya kuwa na kinyongo. "Chukizo" ni jambo linalochukiza, jambo linaloudhi, jambo la kukirihisha.

Chuki za Simba na Yanga zimekuwa ahueni (nafuu anayopata mtu baada ya kupungukiwa na matatizo) kwa timu ngeni zinazokuja Tanzania kupambana na Simba au Yanga. Kwa hiyo timu ngeni huwa na uhakika wa kupata washangiliaji ugenini. Kwa nini mashabiki wa Simba na Yanga wanajidhalilisha hivyo?

**Chuki za Simba na Yanga zimekuwa ahueni (nafuu anayopata mtu baada ya kupungukiwa na matatizo) kwa timu ngeni zinazokuja Tanzania kupambana na Simba au Yanga. Kwa hiyo timu ngeni huwa na uhakika wa kupata washangiliaji ugenini. Kwa nini mashabiki wa Simba na Yanga wanajidhalilisha hivyo?**

Ama kweli wajinga ndio waliwao. Maana yake wajinga ndio wanaopumbazwa au kuliwa. Methali hii huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu ambaye ameishia kuchanganyikiwa kwa njia inayoonekana kuwa rahisi sana.

Jumamosi ya leo Simba ya Tanzania itakapokuwa ikipambana na timu ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini nchini kwao, watu kiduchu (-enye kuwa na kiwango cha chini cha udogo) watakaoishangilia Simba ni wachache wanaoishi Afrika Kusini. Kwa muktadha huo, watakaofaidika ni timu ya Kaizer Chiefs na si Simba inayotoka Tanzania, hivyo ushindi wa Simba utategemea ubora wake dhidi ya timu ya nyumbani yaani Afrika Kusini.

Bendera ni kitambaa chenye rangi au nembo maalumu kinachotambulisha nchi, shirika, chama au jumuiya fulani. Kwa hiyo bendera zinazopeperushwa kwenye milingoti miwili uwanjani wakati wa mechi za timu mbili za nchi tofauti, ni za timu mbili za mataifa mawili zinazopambana -si za klabu.

Taifa ni nchi ya watu wote wanaoishi ndani yake. Jumuia ya watu wenye historia moja, utamaduni mmoja, mfumo wa uchumi na siasa chini ya utawala mmoja. Huu ndio ukweli wenyewe kwa nchi zote duniani.

Kama ndivyo, kwa nini mashabiki wa timu zetu za Simba na Yanga huzishangilia timu ngeni zinapokuja nchini kucheza na timu hizo? Ujinga ni hali ya mtu kutojua jambo fulani. Kwa nini mashabiki wa Simba na Yanga wanatudhalilisha kiasi cha kutufanya tudharaulike na watu wa mataifa mengine? Tunajifedhehesha wenyewe!

Kumbe ndo maana wahenga walituachia methali isemayo: "Udugu wa nazi hukutania chunguni." Hutumiwa kuwapigia mfano watu wasioweza au wasiopenda kushirikiana hadi inapokuwa wakati m-baya sana na wanapokuwa wamechelewa. Yafaa kutambua faida ya kushirikiana ili tuondokane na ubozi (upumbavu) uliokithiri.

Kwa hali hiyo mashabiki wa Simba na Yanga wanapaswa kutambua kwamba zinaposhangilia timu ngeni zinapocheza na timu zetu hufanya tuchekwe na kudharauliwa sana na wageni. Tusijifanye hamnazo kwa kupuuza mambo na kujidai hatuelewi!

Naitakia Simba kila la kheri kwenye mchezo wao dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini leo ili iwe rahisi kwao kwenye mchezo wa marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI PICHANI

# EID EL FITRI KATIKA PICHA



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiwahutubia waumini wa Dini ya Kiislamu wakati wa swala ya Eid El Fitri, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waumini wa Dini ya Kiislam, wakiwa katika swala ya Eid El Fitri, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akijadiliana jambo na Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Abubakar Zubeir Ally na Sheikh Khamis Mataka, baada ya swala ya Eid El Fitri, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Sheikh wa Mkoa wa Shinyanga, Ismail Makusanya (kulia), akiongoza swala ya Eid El Fitri katika viwanja vya Sabasaba, mkoani humo, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**



Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustafa Rajab Shaaban, akikabidhi msaada wa mchele kwa wasiojiweza wakiwamo wajane, yatima na wazee wapatao 400, baada ya swala ya Eid El Fitri, katika Msikiti wa Gaddafi, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Waumini wa Dini ya Kiislam Zanzibar, wakifuatilia hotuba ya swala ya Eid El Fitri, iliyosomwa na Sheikh Abdulraham Said Abduulla (hayupo pichani), katika viwanja vya Maisara Suleiman, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Shaka atamba CCM itashinda Kigoma

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema tathmin ya awali katika uchaguzi mdogo majimbo ya Muhambwe na Buhigwe, inaonyesha watashindwa kwa zaidi ya asilimia 80.

Chama hicho kilifanya uzinduzi wa kampeni za ubunge Muhambwe Mei 4 na Buhigwe Mei 5 mwaka huu, kikiongozwa na Waziri Mkuu na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa, Kassim Majaliwa.

Uchaguzi huo mdogo umetangazwa na NEC kutokana na kufariki dunia kwa Mbunge wa Muhambwe, Atashasta Nditye na Mbunge wa Buhigwe, Dk. Philip Mpango kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais.

Shaka akizungumza na waandishi wa habari mkoani Kigoma juzi, alisema tathmini ya awali imeonyesha katika majimbo hayo CCM itashinda si chini ya asilimia 80 kwa kuwa chama hicho ni baba wa mageuzi ya demokrasia nchini.

Alisema CCM itashinda Buhigwe na Muhambwe kwa haki, amani na utulivu na sababu za ushindi ni nyingi ikiwamo imani kubwa walionayo wananchi kwa Rais Samia Suluhu Hassan na CCM.

Shaka alisema CCM imedhihirisha kivitendo uwezo wake mkubwa wa kuwatumikia wananchi katika awamu zote za uongozi.

Alisema kazi kubwa ya kisera na utekelezaji wa miradi na kuondoa kero imefanyika chini ya CCM kwenye majimbo ya Muhambwe na Buhigwe, hivyo ushindi wa CCM ni jambo lisilo na shaka wala wasiwasi.

Alisema mfumo wa kampeni kwa wagombea wao ulijielekeza katika kufanya mikutano midogo, kukutana na kuzungumza na makundi ya kijamii katika maeneo yao, makazi na vijiji vyao.

Shaka alisema chini ya uenyekiti wa CCM wa Rais Samia, wataendelea kuvilea vyama vya siasa nchini ili viweze kufanya siasa safi na zenye tija kwa Taifa badala ya kufanya siasa za danadana kwa kuwa wote wanajenga nyumba moja na hakuna sababu ya kugombeana fito.

"Ikumbukwe kuwa tokea siasa za nchi hii kuanzia TANU na ASP hatimae CCM, chama chetu hakijawahi kufanya makosa katika mambo ya msingi yanayohusu maslahi ya taifa, hivyo tunakumbusha kuwa uchaguzi wa Buhigwe na Muhambwe umebeba maslahi mapana ya taifa.

"Kwa maana hiyo, unakwenda kuzalisha wabunge wanaokwenda kumuunga mkono Rais Samia katika kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi, kijamii na kisiasa hivyo hatuwezi kufanya makosa," alisema Shaka.

Alisema wamejipanga kuhakikisha wanachama wao wote waliojiandikisha wanajitokeza kwa wingi katika vituo vya kupigia kura na kuwachagua wagombea ubunge wanaotokana na chama chao.

Shaka alitoa wito kwa vyama vingine na wananchi kwa ujumla kuendelea kudumisha amani, usalama na utulivu ambao umekuwapo wakati wote wa kampeni zetu.

# Jafo atoa siku 10 mkurugenzi kuusajili mradi wa machinjio

**Na Mwandishi Wetu,**
KIGOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ametoa siku 10 kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigoma kuhakikisha anasajili mradi wa ujenzi wa machinjio ya kisasa, ili upate cheti cha Tathmini ya Mazingira.

Akiwa katika siku ya pili ya ziara yake mkoani Kigoma, Jafo juzi alitembelea Machinjio ya Manispaa ya Kigoma na kubaini ujenzi unaendelea bila kufuata taratibu za kimazingira kwa kuwa hauna Cheti cha Tathmini ya Athari ya Mazingira.

"Ninaagiza mradi huu usajiliwe mapema iwezekanavyo, na lengo la kufanya hivi si kupata cheti tu bali ni kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala muhimu ya kuzingatia katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira," alisisitiza.

Waziri Jafo alisema endapo Manispaa ya Kigoma itashindwa kusajili mradi huo wa machinjio ya kisasa kwa kipindi tajwa, atasitisha ujenzi huo.

"Hivi sasa kuna mfumo wa kusajili miradi kwa njia ya mtandao na miradi yote ninaiona hapa kwenye tablet yangu sasa ikifika tarehe Mei 25 mwaka huu sijaona mradi wenu, nitasitisha ujenzi wenu," alionya.

Waziri Jafo pia aliwataka wawekezaji kote nchini kusajili miradi yao ili ikidhi vigezo vya kupatiwa cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira kinachoainisha namna bora ya kupunguza madhara ya kimazingira yatokanayo na utekelezaji wa miradi.

Katika hatua nyingine, Jafo alisema azma ya serikali ni kuhakikisha inahamasisha wawekezaji kuwekeza katika uzalishaji wa nishati mbadala ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Waziri Jafo aliyasema hayo mara baada ya kutembelea Mradi wa Nishati ya Jua na kuridhishwa na uzalishaji rafiki kwa mazingira ambao uzalisha kiasi MW moja kwa sasa huku lengo likiwa ni kuzalisha MW 4.8 kufikia mwaka 2025.

Alisema umeme unaozalishwa kutoka katika Mini-grid ya Kigoma una faida kubwa kimazingira kwa kuwa unapunguza matumizi ya umeme wa mafuta ambayo gharama yake ni kubwa na kupongeza uongozi wa Mkoa wa Kigoma kwa kutumia Green Power.



Upanuzi na utoaji mchanga uliojaa ukiendelea ili kurahisisha maji kupita kwa urahisi kwenye Mto Msimbazi, eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Makamu Rais ahimiza wananchi kuchapa kazi

**Na Mwandishi Wetu,**
**KIGOMA**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewataka wakazi wa Kigoma kufanya kazi kwa uadilifu kwa mustakabali wa maendeleo ya taifa, ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu.

Katika hotuba iliyosomwa jana kwa niaba yake na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, Dk. Mpango alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Kigoma kufuatilia maombi ya ardhi kufanikisha shughuli ya kilimo cha zao la mchikichi.

Katika Baraza la Eid lililofanyanyika katika Stendi Mpya ya Kigoma, Dk. Mpango aliwataka wana Kigoma kuendelea kuliombea taifa ili liendelee kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.

"Tukaendeleze amani, upendo, mshikamano kwa yale tuliyoyafanya ndani ya kipindi cha siku 30 za mfungo, tuendelee kuliombea taifa letu ili yote tuliyopanga kutekeleza yaweze kukamilika kwa wakati," alisema.

Dk. Mpango pia aliwataka Watanzania kupendana bila kujali tofauti za dini zao.

Katika baraza hilo, Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Kigoma, lilimwomba Makamu wa Rais kuwapatia ardhi kwa ajili ya kutekeleza kilimo cha michikichi na kujenga zahanati itakayogharimu takriban Sh. bilioni moja.





Baadhi ya waumini wa Dini ya Kiislamu, wakishiriki Swala ya Eid El Fitri, katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watoto wenye ulemavu wampa Samia mambo 4

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameombwa mambo manne na baraza la watoto wenye ulemavu, ikiwamo kuharakisha uundwaji wa mtaala wa lugha ya alama inayofundishwa shuleni.

Rai hiyo ilitolewa jana na Grace Livingstone alipokuwa akisoma risala ya baraza hilo Mkoa wa Dodoma kwa Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa huo, Nathalis Limuma, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa, Dk.Binilith Mahenge, kwenye kongamano la uzinduzi wa mradi wa elimu jumuishi, jijini hapa.

Livingstone alisema hatua hiyo itawezesha lugha hiyo kutumika rasmi kimawasiliano ili watoto viziwi wapate elimu kwa urahisi.

Alitaja mambo mengine waliyoomba kwa Rais ni kuhakikisha mkakati wa elimu jumuishi utekelezwe kwa vitendo katika ngazi za halmashauri na shule pamoja na kusimamia utekelezaji wa sheria za watu wenye ulemavu ili kulinda haki na ustawi wa watu hao.

Pia alisema halmashauri zote ziongeze bajeti kwa shule jumuishi ambazo watoto wenye ulemavu wanasoma.

"Hii ni kutokana na ukweli kwamba vifaa na nyenzo za kujifunzia na kufundishia ni ghali, ukiangalia hapa vifaa tunavyotumia sisi watoto wenye ulemavu na ukilinganisha na gharama za wenzetu wasiokuwa na ulemavu, utaona sisi vifaa vyetu ni gharama kubwa, hivyo tunamuomba Rais Samia Suluhu Hassan, aongeze 'capitation grant' mara mbili au zaidi ili kukidhi mahitaji yetu ya kujifunza shuleni," alisema.

Akizungumzia kero mbalimbali zinazowakabili, Livingstone alisema kuna uhaba wa shule zinazokubali kupokea na kuwafundisha, kukosekana vifaa na nyenzo, walimu wenye utaalamu wa elimu jumuishi.

"Kukataliwa, kubaguliwa na kutengwa kwa watoto hao kuanzia ngazi ya familia hadi taifa, suala ambalo limekuwa wakikosa huduma stahiki na maendeleo ya malezi na makuzi nya mtoto," alisema.

Naye, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa huo, Nathalis Limuma, alisema serikali inatambua matatizo yanayowakabili watu wenye ulemavu wakiwamo watoto.

Alisema kuwa kutokana na matatizo hayo viongozi wa ngazi ya chini hadi taifa wanatakiwa kuzijua sheria zitakazosaidia kutatua kero zao.

Aliagiza halmashauri kusimamia na kulea mabaraza ya watoto ili kuwaandaa viongozi wenye maadili mema.

# Wajasiriamali wapewa siri ya uvuvi wenye tija

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka wajasiriamali wa uvuvi kuzingatia sheria na taratibu zilizopo ili kuvua kwa tija.

Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi, Emmanuel Bulayi, alitoa ushauri huo kwenye warsha ya kuwajengea uwezo wavuvi iliyojumuisha wataalam wa sekta hiyo.

Alisema matumizi ya rasilimali za uvuvi nchini yanapaswa kusimamiwa ili kuendelea kuwapo hadi vizazi vijavyo.

Alibainisha wavuvi wanapaswa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na serikali katika matumizi ya rasilimali hizo.

"Tunafahamu jamii inayoishi karibu na rasilimali za uvuvi inategemea biashara hiyo, nawaomba baada ya warsha hii muende kutoa elimu kwa wavuvi wengine," alisema Bulayi.

Alisema anaamini baada ya warsha hiyo wavuvi watakujwa na sera mpya ya uvunaji ambayo itasaidia kuwainua kiuchumi, kuvua kwa tija na kusaidia sekta hiyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa.

Mvuvi Ester Kunambi, aliomba serikali kufungulia uvuvi wa mchana wa dagaa na samaki ili uwasaidie kujiinua kiuchumi ikiwamo kurejesha mikopo waliyoikopa.

Kunambi alisema uvuvi wa dagaa majira ya mchana ulikuwa unawasaidia kupata bidhaa hiyo kwa wingi pamoja na samaki, lakini baada ya kuzuia suala hilo limekuwa vigumu kwao kurejesha mikopo ya asilimia 10 kwa wakati waliokopeshwa na halmashauri.

"Tunaiomba serikali itusaidie kurejesha uvuvi wa mchana, tunaahidi kufuata sheria za uvuvi kama zilivyowekwa na serikali," alisema Kunambi. Alisema serikali inapaswa kuwaangalia wavuvi wadogo ili nao wapige hatua katika uvuvi, ambao utawasaidia kujiinua kiuchumi.

Naye, Ofisa Mwandamizi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Upendo Hamidu, alisema serikali imejitahidi kuziboresha rasilimali za uvuvi ili kutumiwa na wavuvi.

Alisema mkutano huo ulijumuisha wataalamu kutoka sehemu mbalimbali ili kujadili namna ya kuwasaidia wavuvi kupata kipato kitakachowainua kiuchumi.

# COSTECH sasa yajipanga kuboresha bunifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), imejipanga kuziboresha bunifu za wabunifu ili zikidhi viwango vya kimataifa na kuchangia pato la taifa.

Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, aliyasema hayo jijini hapa, baada ya agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuzitaka taasisi zinazohusika na kuendeleza bunifu za wabinifu kuhakikisha zinawasaidia kuboresha kazi zao.

Alisema COSTECH imejipanga kuhakikisha bunifu zilizowasilishwa katika mashindano ya ubunifu (MAKISATU) yaliyomalizika hivi karibuni jijini Dodoma zinaboreshwa na kuendelezwa.

"Nimefurahi kuona mwaka huu wabunifu wamewasilisha vitu vikubwa sana katika MAKISATU, hii inaonyesha jinsi gani wanavyoelewa pale wanapopewa marekebisho kwa ajili ya kuboresha kazi zao," alisema Dk. Nungu.

Alibainisha kuwa wao wameridhika na namna wabunifu walivyozingatia maboresho waliyopewa na kubuni, na kwamba wengi wamepata ushindi wakati wa kilele ya kufunga kwa mashindano ya MAKISATU. "Tumefurahi kuona mashindano hayo ambayo hata Waziri Mkuu ameshuhudia na kukubali kuwa Tanzania kuna watu wana vipaji na wenye bunifu nzuri za Kisayansi ambazo," alisema.

Alisema ume hiyo imejipanga kuwaendeleza wabunifu hao kwa kuwapa muongozo na malezi na kuboresha kazi ambazo wamebuni ili kuwa wajasiriamali na wabunifu wakubwa hapo baadae.

"Lengo lao ni kuona wabunifu wanapiga hatua katika kazi zao za ubunifu wanazofanya, ambazo zitawasaidia kujiinua wao kiuchumi, lakini pia kulitangaza taifa katika nchi mbalimbali watakazofanikiwa kwenda kushiriki maonyesho ya kimataifa," alisema.

Akifunga maonesho ya MAKISATU, Majaliwa aliagiza COSTECH, SIDO, VETA na Don Bosco kuhakikisha wanakuwa karibu na wabunifu hao kwa kuwaendeleza katika mawazo yao ya ubunifu ikiwamo kuziendeleza bunifu zao.

Majaliwa alisema taasisi hizo ndizo zimepewa dhamana na serikali kuhakikisha wabunifu hao wanaendelezwa na kukua ili bunifu hizo ziwe na tija katika taifa.



# Angalizo matumizi bidhaa za tumbaku

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Dk. Omar Dadi Shajak, ameitaka jamii kuacha kutumia bidhaa zinazotokana na tumbaku.

Angalizo hilo limetolewa kutokana na bidhaa hizo kuwa kichocheo kikubwa cha maradhi yasiyoambukiza, ambayo yamekuwa tishio kubwa duniani.

Akifungua mafunzo ya waandishi wa habari kuhusu Kanuni ya Tumbaku ya mwaka 2016, alisema matumizi ya tumbaku yamekuwa yakipoteza maisha ya watu wengi hivi sasa.

Katika kupiga vita matumizi ya tumbaku, Dk. Shajak aliwataka wazazi na walezi kuacha tabia ya kuwatuma watoto dukani kununua sigara, kwani kufanya hivyo ni kuwahamasisha kuingia katika mkumbo wa kuvuta sigara.

Shajak aliwashauri wavutaji wa sigara kufuata kanuni ya tumbaku kwa kuacha kuvuta sigara katika mikusanyiko ya watu kwa lengo la kuwanusuru wasiotumia kupata athari inayotokana na moshi wa mtumiaji.

Alisema pamoja na matangazo yanayotolewa na wazalishaji wa sigara kuhusu athari zinazotokana na uvutaji wa sigara na bidhaa zinazotokana na tumbaku, bado matumiza ya bidhaa hizo ni makubwa.

Naye, Kaimu Meneja wa Kitengo cha Maradhi yasiyoambukiza, Omar Abdalla, alisema vifo vinavyotokana na maradhi yasiyoambukiza vimekuwa vikiongeza kwa kasi ya kutisha.

Alisema kati ya watu kumi wanaofariki Zanzibar, sita hufariki kutokana na maradhi yasiyoambukiza, na kwamba chanzo kikubwa ni kutumia bidhaa zinazotokana na tumbaku na mlo usiokamili.

Aliyataja maradhi hayo ni shindikizo la damu, kisukari, saratani ya shingo ya kizazi, tenzi dume, maradhi ya moyo, maradhi ya akili na maradhi ya njia za hewa.

Ofisa wa Kitengo cha Maradhi yasiyoambukiza Zanzibar, Zuhura Saleh Amour, alisema zaidi ya watumiaji tumbaku milioni nane hufariki dunia kila mwaka duniani, ambapo milioni 1.2 sio watumiaji, lakini wanaathirika kwa kukaa karibu na watumiaji.



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis Juma akifungua warsha ya ukusanyaji wa takwimu za namna ya kutoa mrejesho katika masuala ya HIV na elimu ya afya ya uzazi na jinsia, iliyoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la masuala ya Elimu, Sayansi na Utamaduni la UNESCO, mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wazanzibari wapewa matumaini ajira 21% taasisi za Muungano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema suala la malalamiko ya mgawanyo wa ajira kwa Zanzibar ya asilimia 21 katika taasisi za Muungano litaondoka na kubakia kuwa historia endapo waliopewa dhamana ya kulisimamia watalitekeleza.

Aliyasema hayo juzi, ofisini kwake wakati akizungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wa Tanzania), Mohamed Mchengerwa, aliyembatana na viongozi waandamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jasmii (TASAF) na wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Alisema suala hilo kwa vile halimo katika kero za Muungano, linapaswa kusimamiwa vyema katika utekelezaji wake ili malalamiko yanayotolewa na baadhi ya wananchi yafikie ukomo.

Aliwashauri wataalamu na watendaji wanaosimamia masuala hayo watumie taaluma zao katika kuwaelimisha wananchi mbinu na namna watakavyotumia fursa zinazotokea katika ajira kupitia mfumo wa Teknolojia na Habari na Mawasiliano. "Nafarijika kuona suala hili tayari limeanza kufanyiwa kazi kwa vile hata ndani ya vikao vya Baraza la Wawakilishi limekuwa likiulizwa na Wajumbe wa Baraza hilo. Inaonekana hata wewe mwenyewe binafsi Waziri umelisikia au kupata taarifa zake," alisema Hemed. Akizungumzia TASAF, Hemed alionya kwamba mtu au kiongozi atakayeamua kugusa fedha zilizotengwa na mfuko huo kwa ajili ya kaya maskini kinyume cha utaratibu, atalazimika kuwajibishwa mara moja.

Alisema fedha hizo zinazotolewa na Serikali lazima ziheshimiwe kwa vile zimetengwa na kulenga watu maalum ili ziwafikie Watanzania walio wengi katika maeneo mbalimbali hasa vijijini, ambao baadhi wana kipato duni.

Naye Waziri Mchengerwa alisema Wizara anayoiongoza imeandaa utaratibu utakaotoa fursa ya kuwasajili wanafunzi wote wanaomaliza masomo ya sekondari na vyuo Zanzibar. Alisema hatua hiyo muhimu aliyoahidi kuifanyia kazi, itarahisisha kuwapata vijana wa Zanzibar pale zinapotokea fursa za ajira kwa taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa vigezo, sifa na elimu zao zitakazokwenda sambamba na ajira husika.

Waziri Mchengerwa alibainisha kwamba suala la mafunzo kwa watumishi wa umma litazingatiwa kwa kina kupitia Mfumo wa Ushirikishwaji wa pamoja kati ya vyuo vya utumishi wa umma vya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa upande wao viongozi waandamizi wa TASA, MKURABITA, pamoja na Sekreterieti ya Utumishi wa Umma na Ajira, walisema lengo la kuanzishwa kwa taasisi wanazozisimamia ni kusaidia kuondoa umaskini kwa Watanzania walio wengi.

# Sababu elimu ya afya, uzazi kutolewa shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis Juma, amesema ni muhimu elimu ya afya ikiwamo afya ya uzazi kutolewa shuleni kwa sababu wanafunzi wengi wanaingia katika uhusiano kabla ya kumaliza msomo.

Aliyasema hayo wakati alipofungua warsha ya ukusanyaji wa takwimu, namna ya kutoa mrejesho katika masuala ya HIV pamoja na elimu ya afya ya uzazi na jinsia, ambayo imeandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni la (UNESCO).

Alisema madhara makubwa wanayapata wanafunzi wanapojiingiza katika uhusiano, hivyo elimu hiyo itasaidia kujua athari zake na kuacha kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi wakiwa bado na umri mdogo.

Alisema umeonekana upungufu katika kutoa elimu kutokana na jinsi inavyotolewa baada ya tatizo kutokea. Alisema warsha hiyo ni muhimu sana na itaisaida serikali katika kupanga mipango mbalimbali hasa ikizingatia hivi sasa baada ya kuondolewa ugatuzi, Wizara ya elimu ina kundi kubwa la watoto na wa rika la tofauti.

Aidha, alisema ni muhimu kwa Taifa kuangalia ni maeneo yapi yanaweza kukusanywa takwimu kwa lengo la kutatua matatizo yaliokuwapo hasa ya kielimu pamoja na kuyafanyia kazi kwa maendeleo ya watoto.

Ofisa Elimu na Afya kutoka ofisi za UNESCO Dar es Salaam, Mathias Herman, alisema kwa mujibu wa nakala ya Waziri wa Elimu ya mwaka 2003, iliazimiwa kuwa wizara za elimu zikusanye takwimu juu ya masuala ya HIV na jinsia, na kwamba hiyo inatokana na mchango wa elimu kuwa mtambuka.

Alisema mchango huo kidunia ulikuwa hautambuliki vizuri, kutokana na kutokuwa na njia mbadala za kujulikana kimataifa.

Aliwataka wakufunzi hao kuyafanyia kazi mafunzo waliyopewa na kuhakikisha wanakusanya takwimu vizuri katika masuala ya udhalilishaji na HIV kwa wanafunzi wanaokumbwa na kadhia hizo.

Ofisa Elimu na Afya kutoka UNESCO ofisi ya Zanzibar, Hasina Salim Bukheti, alisema hivi sasa wizara ya elimu ina uhaba wa taarifa juu ya masuala ya udhalilishaji katika takwimu na taarifa za afya katika dodoso la elimu, hali inayowafanya kushindwa kuripoti vyema katika dodoso la dunia. Kutokana na hali hiyo, wameona umuhimu wa kufanya warsha hiyo ili waweze kujifunza kwa kutumia muongozo wa dunia kwa lengo la kujua njia zipi zinaweza kuwafaa katika kuzitumia katika takwimu zao.





Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MEI 15, 2021



# WAMEUMANA

## Zari, Wema wapeana makavu kweupee

HALI ya hewa imechafuka kati ya warembo wawili maarufu nchini, Wema Sepetu na Zarina Hassan, maarufu kama 'Zari' baada ya kurushiana maneno makali.

Wawili hao ambao wote walikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamuziki nyota, Diamond Platnumz, wameibua vita hiyo baada ya kila mmoja kuonekana kuchoshwa na chokochoko zinazotoka kila upande.

Pengine mashabiki wa kila upande wanaweza kulaumiwa kwa kuchochea moto huo, baada ya kuwapandisha hasira kutokana na maswali wanayowauliza.

Kwa mfano wakati Wema Sepetu alipotangaza kupotewa na mbwa wake, mashabiki hao walimuuliza Zari kama na yeye kapoteza na kutoa donge nono ili kumtafuta.

Zari bila kuchelewa alijibu kwamba mbwa huyo hakupotea bali Wema anatafuta kiki.

Jibu hilo ni kama halikumfurahisha Wema na ndipo kupitia chombo kimoja cha habari, alisema kauli hiyo ni sawa na mwizi anayehisi anataka kuibiwa.

"Ukiwa mwizi unahisi kila mtu mwizi, ukiwa muongo unahisi kila mtu muongo na ukiwa muhuni utahisi kila mtu muhuni, nadhani nimeeleweka," alisema baada ya kuulizwa anajisikiaje kuonekana kama alidanganya.

Bila ya kuchelewa Zari kupitia Istagram, alimjibu mshabaki wake kwa kumfananisha Wema sawa na mwanamke aliyeishiwa na anahitaji msaada wa chakula.

"Nipo kwenye ramadhani natoa msaada, nataka kumsaidia Wema apate chakula, sasa amebaki kichwa tu anatakiwa kula chakula hiki cha bure ili awe vizuri" aliandika.

Hata hivyo, bado haijafahamika kwa nini warembo hao sasa hivi ameamua kutupiana maneno, huku baadhi ya mashabiki wao wakieleza pengine inatokana na kila mmoja kumuonea wivu mwenzake.

BASI SAWA

## Mwasiti unafaa kuelimisha vijana

MSANII mkongwe wa muziki wa Bongo Fleva, Mwasiti, amejikuta akiwa kama mtaalamu wa afya baada ya kusema kasi ya maambukizi ya UKIMWI nchini inatisha.

Mwasiti ameandika hayo katika ukurasa wake wa Instagram, baada ya Tume ya kuthibiti UKIMWI (TACAIDS), kutoa takwimu mpya inayoonyesha kuongezeka kwa idadi ya watu wanaopata maambukizi.

"Asilimia kubwa ya vijana mambo yao yanafanana, tuambiane ukweli kwa sababu tulipofika sio sehemu nzuri ya kujivunia, vinginevyo kama hatuongei athari itakuwa kubwa zaidi ya tunavyofikiria, miaka 14 mpaka 24 ni vijana wadogo wanaoambilika, hili janga lipo tusichukulie poa".



## Ferooz kumbe mjanja

MWANAMUZIKI wa siku nyingi katika muziki wa kizazi kipya, Ferooz, amesema anajiona ni mtu mwenye bahati baada ya kunusurika kuambukizwa UKIMWI wakati anatamba na nyimbo zake.

Amesema wakati akiwa katika shoo yake jijini Mwanza, alikutana na wanawake wawili ambao walijipendekeza kwake, lakini kabla hajachukua uamuzi aliambiwa asiwakaribie kwani wamepata maambukizi.

"Niliwahi kwenda kwenye show Mwanza, kuna pisi ikawa imeniganda sana yaani inanifuata fuata mara anataka tupige picha nikawa sielewi kwanini inaniganda,kuna washikaji wakaniambia hiyo pisi imeathirika isije ikakuua, nikajua wana wanaona wivu" amesema.





## Young Dee anakshi Albam yake mpya

MWANAMUZIKI wa Hiphop, Young Dee, anafanya mambo mazito katika Albam yake mpya baada ya kumshirikisha dada wa rapa wa Marekani, Young Thug, katika moja ya nyimbo zake.

Katika ujumbe wa sauti uliowekwa kwenye ukurasa wake wa Instagram, rapa huyo alimpongeza Dolly kwa kufanya vizuri ndani ya Albam hiyo.

Young Dee amefanya kama ilivyokuwa kwa Young Thug, kwa kumshirikisha Dolly ambaye yupo chini ya lebo ya "Young Stoner



## Serikali kupanga bei elekezi kwenye filamu

SERIKALI imekuja na mpango wa bei elekezi ya kuuza kazi za sanaa nchini kutokana na kuonekana kudorora kwa tasnia hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk Kiagho Kilonzo, katika hafla ya uzinduzi wa tamthilia ya 'We Men' alisema wazo hilo limeibuka baada ya wasanii wengi kuacha kazi hiyo kutokana na kulipwa ujira usioendana na kazi wanazozifanya.

"Hali hiyo inawavunja moyo wasanii na watayarishaji kutokana na malipo yake hayafiki hata robo ya kazi anayoifanya, wasanii wetu wanatakiwa kunufaika na kazi zao maana ndio kiinua mgongo chao au jasho la kazi zao," amesema.

Ameongeza kuwa wakati mwengine wasanii wanafanya kazi huku malipo hayaendani na gharama za uandaaji wa filamu jambo ambalo linachangia kurudisha nyuma tasnia hiyo nchini.

Siku ya Mei 12 ilitoka takwimu mpya za Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI ambapo taarifa zinaeleza kuwa watu wa umri wa miaka 15 hadi 24 ndiyo wanaongoza kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

## HAWA WANAIMBA MUBASHARA

**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na wasanii wengi nchini ambao wanasaidiwa mno na 'maprodyuza', huku wenyewe wakiwa hawawezi kupiga muziki laivu.

Wasanii wengi wa Watanzania ukitaka kuwaweza, kuwe na muziki wa laivu na piga hata nyimbo zao zile zile kwa vyombo, halafu waambie waende kuimba, utashangaa.

Unaweza kudhani kuwa siyo yule aliyeimba ngoma hiyo. Ukweli ni kwamba wasanii wengi wanaingia studio kwenda kuimba tu. Tena wakati mwingine wanaimba vibaya, lakini wasaidiwa na prodyuza na makompyuta yake.

Halafu mirindimo inatafutwa na prodyuza. Msanii anakuja kuishtukia ngoma yake tayari imeisha huku kila kitu akiwa amefanyiwa.

Lakini kuna watu huwa wanapiga nyimbo za wasanii kwa kutumia vyombo halisi vya muziki. Sasa mwite msanii mwenyewe aliyeimba wimbo huo apande jukwaani, anashindwa kuimba kama vile alivyorekodi studio.

Ni kwa sababu kule alikuwa anarudia sana. Sauti imerekebishwa na vitu vingi vya kiufundi.

Ukweli ni kwamba wana matatizo ya 'key', yaani ufunguo. Hata ngoma yake mwenyewe anakuwa hajui ameimba key gani.

Ataimba kwa sauti ya juu sana kuliko vyombo vinavyipigwa au chini na kusababisha wimbo kutokuwa kwenye hali yake ya kawaida.

Wana matatizo pia ya 'timing'.  Kujua hapa ndipo pa kuingilia kuimba na hata pa kutokea.

Ndiyo maana baadhi ya wasanii wakajiongeza na kuanza kujifunza kupiga muziki laivu.

Hawa ukiwapigia nyimbo zao kwa kutumia magitaa, wataimba tu hawana wasiwasi wowote hata ukiwaamsha usiku wa manane.

Leo tunawataja wasanii ambao ni kama wanamuziki tu, wana uwezo mkubwa wa kuimba muziki wa 'laivu' bila matatizo.

**Lady Jaydee**

Ni msanii mkongwe nchini ambaye kwa sasa unaweza kabisa kumwita ni mwanamuziki.

Katikati ya miaka ya 2000 alipokwenda nchini Uingereza na kina King Kiki na marehemu Ndala Kasheba, alikutana na changamoto ambayo ilimfanya kuanza kujifunza kupiga muziki laivu.

Ni kwamba wakongwe kina King Kiki ndiyo waliokubaliwa zaidi kwa sababu walipiga muziki laivu, na wao walikuwa wanatumia 'play back' yaani CD. Wazungu walikuwa hawapenzi wa hilo. Wao walitaka muziki wa laivu. Mwanamuziki Oliver Mtukudzi kutoka Zimbabwe ambaye naye alikuwa huko, ndiye aliyemshauri Lady Jaydee kupiga muziki wa laivu kwa sababu ana uwezo mkubwa na sauti nzuri. Aliporejea alinunua vyombo na kuunda bendi yake ya Machozi. Kwa sasa anaimba laivu kama kawaida.

**Banana Zorro**

Unaweza usishangae sana kwa sababu huyu ni mtoto wa mwanamuziki Zahir Ally Zoro aliyepigia bendi za JKT Mafinga, maarufu kama Kimulimuli, Sambulumaa na nyingine nyingi.

Alijiingiza kwenye muziki wa kizazi kipya, lakini yeye akiwa na uwezo mkubwa wa kuimba laivu akipigiwa vyombo. Pia anajua kupiga gitaa, hivyo ni mwanamuziki aliyekamilika.

**Ali Kiba**

Katika hali inayoonyesha kuwa jamaa ni mbishi na pia ana kipaji halisi cha muziki, Ali Kiba ni mmoja wa wasanii mwenye uwezo mkubwa wa kuimba laivu. Kuna baadhi ya matamasha yake, nyimbo zake nyingi amekuwa akiziimba huku akiwa anapigiwa magitaa na vinanda na kuziimba vile vile kama zilibyorekodiwa studio, kitu ambacho ni ngumu mno kwa wasanii wengi ambao amekuwa tu akishika 'mic', na kusema yo yoo, nyimbo zao zikipigwa 'play back', yaani zile zile walizorekodi studio.

**Peter Msechu**

Huyu pia ni mmoja wa wasanii ambao wana uwezo na ujuzi mkubwa wa kusimama jukwaani na kuimba muziki wa laivu bila matatizo yoyote na amekuwa akifanya hivyo siku zote.

**Zuchu**

Ni msanii wa kike mwenye uwezo mkubwa wa kuimba katikati ya magitaa, vinanda na vyombo vingine vya muziki laivu bila shida yoyote. Inawezekana kwa sababu na yeye ametoka kwenye familia ya muziki kwani baba yake Ustaadhi Othman Sudi na mama yake Hadija Kopa walikuwa ni wanamuziki wa taarab. Muziki huo ni lazima uimbe laivu, vinginevyo umekushinda. Hauna kuweka CD wala flash. Kwenye maonyesho yake amekuwa akiteka mashabiki akiimba laivu, kitu ambacho kimemfanya kuwa na mashabiki wengi nchini.



## Vichwa Maji: Chungu ya penzi, hupozwa kimapenzi

**Na Adam Fungamwango**

SIKU zote kwenye dunia hii, mapenzi ndiyo kitu cha kwanza, mengine yanafuata. Watu wanafanya kila kitu ili wapendwe. Dawa ya penzi hakuna. Huponywa tu na yule aliye moyoni mwako. Hasira ya mapenzi soku zote humalizika kwa mapenzi.

Kwa maana hiyo ni kwamba mara nyingi wapendanao waachwe kama walivyo. Hata kama wakigombana, usiingilie kabisa ugomvi wao. Mmoja akisema anaondoka au anadai talaka kama ni ndugu au jirani, jitenge kuwa upande wa yoyote yule. Amua tu kama wanapigana au kutukanana. Lakini mengine kaa kimya. Vinginevyo unaweza kuonekana mbaya baadaye.

Kuna wimbo mmoja unasema mambo ua unyumba usiingilie, kwa sababu wakipatana utabaki na aibu. Utamsaidia shoga 'ako aliyepewa talaka na mumewe kufukuzwa kubeba vyombo wakati anaondoka, lakini ukashangaa baada ya siku tatu ukamuona amerudi. Wewe sasa ndiyo utaonekana mbaya ulikuwa na nia ovu ya kutaka kuharibu mapenzi au ndoa ya watu.

'Vichwa Maji' ni filamu iliyochezwa na wasanii Zimwi, Senga, Fetty, Pembe na wengine kuelezea kitu mapenzi ambacho hakipimiki na kitu chochote.

Senga anapita kwa jirani yake Pemba. Anamuona mke wa jirani yake anaingia bafuni. Kama kawaida ya vyoo na mabafu ya uswahilini yalivyo. Senga anaamua kwenda mlangoni kumchungulia.

Wakati anafanya hivyo, Pembe alimuona. Alimnyatia wakati Senga akili yake iko kwa anachokiona ndani ya bafu.



Anamkamata. Akampa kipigo kizito kiasi cha mke wa Pembe pamoja na kufanyiwa udhalilishaji, akamtaka mumewe aache kumuadhibu mwanaume mwenzake. Hiyo ikaamuudhi Pembe na kumwambia huenda wako kwenye njama moja. Ugomvi ukahamia kwa mkewe. Lakini baadaye wakayamaliza kama mtu na mkewe.

Zimwi yeye ni mume bwege. Anampelekea mkewe maji ya kuoga bafuni. Mkewe anaondoka kwenda kwenye starehe, yeye anafua, kuosha vyombo na kupika. Mkewe akirudi anadai msosi.

Siku moja Fetty ambaye ni mke wa Zimwi alirudi na bwana nyumbani. Hilo lilimkera sana Zimwi. Akachonga sana. Lakini mke akampetipeti, yakaisha.



# VictOny atoka ICU, azidi kupata nafuu

RAPA wa Nigeria VictOny, ambaye wiki iliyopita alipata ajali mbaya na kulazwa hospitali kwa ajili ya matibabu, imeelezwa amefanyiwa upasuaji ili kuokoa maisha yake.

Kulingana na maelezo yaliyotolewa na KVLT kupitia mtandao wa Twitter, mwanamuziki huyo anayekuja kwa kasi ameondolewa katika chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU) baada ya upasuaji huo kwena vizuri.

Mwanzoni mwa mwezi huu, rapa huyo akiwa na rafiki zake ndani ya gari, walipata ajali mbaya wakati wakirudi katika sherehe ya kuzaliwa mwanamuziki maarufu Oxlade.



## Iyabo Ojo unachokifanya si haki

MWIGIZAJI nyota wa Nollywood, Iyabo Ojo, ameibua mjadala mkali baada ya kuziweka wazi jumbe alizotumiwa na msanii mwenzake, Yomi Fabiyi, ambazo aliomba radhi baada ya kumshambulia kimtandao.

Fabiyi aliweka jumbe hizo za Ojo ambazo aliwasiliana naye kuomba msamaha, ambapo alikiri kumshambulia kwa kudhamiria.

Kwa kutumia ukurasa wake wa Instagram, Ojo aliziweka jumbe hizo ambazo zilionyesha Fabiyi wakilumbana kuhusu tukio la ubakaji la Baba Ijesha.

## Nani kama Youssou N'Dour

WIKI hii mwanamuziki mkongwe, Youssou N'Dour,ametajwa kuwa msanii tajiri namba moja barani Afrika.

N'dour raia wa Senegal, ana utajiri wa dola milioni 145 hadi 150, kulingana na ripoti mpya ya jarida la African Forbes 2021.

Wanamuziki wengine wanaomfuatia kwa kuwa na fedha nyingi ni Akon anamiliki dola milioni 80, Black Coffee, milioni 60, Wizkid milioni 21 na Davido milioni 20.





## Baba Ijesha azidi kubanwa

KAMISHNA wa Polisi wa Lagos, Hakeem Odumosu, amesema msanii nyota nchini humo, Baba Ijesha, ataendelea kushikiliwa kwa ajili mahojiano.

Mwigizaji huyo kutoka Nollywood, alikamatwa hivi karibuni baada ya kutuhumiwa kumbaka msichana mwenye miaka 14.

Taarifa hiyo imetolewa baada ya kuwapo na tishio la maandamano kupinga jeshi la polisi kumwachia huru msanii huyo baada ya kukamilisha mahojiano.

## Wiki ya Bob Marley

WIKI hii wapenzi na mashabiki wa mwimbaji mashuhuri wa rege, Bob Marley, wamefanya kumbukizi ya miaka 40 tangu kifo chake kilichotokana na saratani.

Marley, amefariki Mei 11, mwaka 1981 katika mji wa Miami nchini Marekani, akiwa na umri wa miaka 36.

Mwanamuziki huyo ni mmoja wa wasanii mashuhuri na wanaotambulika katika historia ya muziki, na vibao vikiwemo No Woman No Cry, One Love, na Redemption Song.



MAKALA

# VUTA NIKUVUTE JERUSALEM

## ■Waisrael, Wapalestina zaidi ya chuki na hasira

Na Mwandishi Wetu

BADO mapigano yanazidi kushika kasi ukanda wa Gaza, polisi wa Israel na wanamgambo wa Kipalestina wanakabiliana vikali kwa kurushiana maroketi na makombora yanayoangushwa na ndege za kivita.

Wimbi hilo jipya ghasia limekumba eneo lote la Israel na ukanda wa Gaza, huku uhasama unazidi kupenya ndani ya jamii ya Wayahudi na Waarabu ambao sasa wameanza kushambuliana mitaani.

Mzozo huu wa sasa unaonekana kuwa tofauti zaidi na huko nyuma, ambapo jamii hizo ambazo zilikuwa zikiishi pamoja licha ya kuwapo na kutoelewa, lakini kinyume chake ndani ya Israel kumegawanyika kati wa Wayaudi na wale Waarabu raia wa nchi hiyo.

Ni wazi kabla ya kuibuka kwa ghasia hiyo, kulikuwa na kidonda kibichi katikati mwa eneo la mashariki ya kati, licha ya kwamba mzozo huo haujawekwa kipaumbele kwa vyombo vya habari vya kimataifa katika miaka ya hivi karibuni.

Pamoja na kuonekana kama kumepoa, bado matatizo ndani ya eneo hilo hayakubadiliki, huku chuki na uchungu ukiendelea kurithisha kizazi hadi kizazi.

Mapigano hayo kati ya Waisraeli na Wapalestina yamesababisha takriban watu 230 kufariki katika eneo la Gaza na watatu nchini Israel kwa muda wa wiki mbili pekee.



Mlipuko wa bomu katika makazi ya Wapalestina baada ya ndege za Israel kushambulia.

**CHANZO NINI?**

Kwa zaidi ya karne moja sasa , Wayahudi na Waarabu wamekuwa wakipigania kumiliki ardhi kati ya mto Jordan na bahari ya shamu.

Israel inawaadhibu Wapalestina tangu taifa hilo lilipobuniwa mwaka 1948, lakini katika mvutano huo haiwezi kujitangaza kuwa mshindi.

Na iwapo mgogoro huo utaendelea hakuna aliye na hakika ni nani atakayekuwa mshindi.

Hakikisho lililopo ni kwamba kila miaka inaposonga mbele mgogoro huo unazidi kukua na kuwa mbaya zaidi.

Pamoja na eneo hilo kuwa na mfumo wa ukuta kwa kipindi cha miaka 25 iliopita, haimaanishi Israel itaondoa wazo la kuufanya mji wote wa Jerusalem kuwa makao yake makuu.

**TATIZO LA JERUSALEM**

Kuzuka kwa ghasia wakati huu kumekuwa ukumbusho kwamba mji wa Jerusalem ambao unaaminika kuwa eneo takatifu unazidi kuchochea hisia za watu wengi.

Utakatifu wa mji huo kwa upande wa Wakristo , Wayahudi na Waislamu sio tu swali la kidini, bali ni la kidunia nzima.

Maeneo matakatifu ya Waislamu na Wayahudi pia ni maeneo ya kitaifa.

Msikiti wa Al Aqsa unatambuliwa na dini za Kiyaudi na Kiislamu kama ni eneo tukufu zaidi.

Kanisa la mtakatifu Sepulcher, pia liko karibu, karibu na kizuizi cha Israel, kinachoheshimiwa na Wakristo wa Palestina.

Hata hivyo, kumekuwa na tishio la kuwaondoa Wapalestina kutoka katika makazi yao katika wilaya ya Sheikh Jarrah.

Eneo hilo ni la Palestina nje ya ukuta wa mji wa zamani, huku ardhi `na mali zikimilikiwa na walowezi kwa msaada wa mahakama za Israel.

Hatua ya kutaka kuwaondoa wakazi hao ilitaka kutimizwa kwa miaka kadhaa na serikali zilizopita ili kutimiza lengo la kuifanya Jerusalem kumilikiwa na Wayahudi.

Hata hivyo, nyumba zilijengwa kwenye ardhi iliyokaliwa ili kuuzunguka mji huo, kwa lengo la kukiuka sheria za kimataifa.

Katika miaka ya hivi karibuni, serikali na vikundi vya walowezi vimefanya kazi kuwapatia Wayahudi wa Israeli nyumba katika maeneo ya Wapalestina karibu na mji wa kale.

**MAPIGANO MAPYA**

Mlipuko mpya wa ghasia ulitiwa mafuta katika wiki za hivi karibuni kufuatia hatua ya Israel kuweka vizuzi kuingia katika msikiti wa Al Aqsa siku ya Ijumaa kabla ya mfungo wa Ramadhani kumalizika.

Hatua hiyo ilisababisha vurugu kiasi ambacho polisi wa Israel waliingia ndani ya msikiti na kuwatawanya waumini kwa maji ya kuwasha na mabomu ya machozi.

Eneo hilo ni takatifu zaidi miongoni mwa waumini wa dini ya Kiislamu baada ya Maka na Madina.

Hatahivyo, kundi la wapiganaji wa Hamas lilichukua hatua za kuionya Israel kuondoa vikosi vyake katika msikiti wa Al-Aqsa na wilaya ya Sheikh Jarrah na baadaye kurusha roketi mjini Jerusalem.

Waziri mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alituma ujumbe wa twitter akisema mashirika ya kigaidi katika eneo la Gaza yalivuka mpaka mwekundu na kuahidi Israel itajibu kwa uwezo mkubwa.

**KUNA SULUHU?**

Mtangazaji wa BBC alimuuliza mkazi mmoja kama ana matumaini siku moja ataona pande hizo mbili zitafikia mwafaka ili kuishi kwa amani.

Hata hivyo, mkazi huyo anasema aliishi Jerusalem kutoka mwaka 1995 hadi 2000 na alirudi katika eneo hilo kila mara. Kupata jibu lakini imekuwa vigumu.

Katikati ya mkutano wa amani wa Oslo uliofanyika miaka ya 90, kulikuwa na matumaini kwa muda mfupi , lakini ni wakazi wa Jerusalem walio katika umri wa miaka 40 ndio walio na ufahamu jinsi amani ilivyoafikiwa.

Viongozi wa pande zote mbili wamekuwa wakikabiliana kisiasa ndani ya maeneo yao , wakijaribu kulinda maslahi yao , huku tatizo kuu la kiongozi wa Palestina na Israel likiwa ni kuleta amani katika eneo hilo. Changamoto hiyo haijaangaziwa kwa undani kwa miaka kadhaa sasa.

**MAPYA YAMEIBUKA**

Makundi mawili yanayoheshimiwa katika eneo la mashariki ya kati kwa kupigania amani , the Carnegie Endowment for International Peace na lile la US / Middle East Project yamechapisha ripoti ya pamoja yakisema kwamba kipaumbele ni kutoa haki sawa na usalama kwa raia wa Palestina na wale wa Israel.

Yanasema kwamba Marekani ni sharti kuunga mkono usawa kamili na haki ya kupiga kura kwa wale wote wanaoishi chini ya utawala wa Israel, sio kuunga mkono mifumo tofauti isiyo na usawa wowote.



Polisi akishuhudia gari likiwaka moto baada ya kushambuliwa na Wapalestina katika mji wa Jerusalem.**PICHA ZOTE :MTANDA**

# Wengi wana matatizo ya akili

## •Hasira, wivu, sonona ni dalili hatarishi

Na Christina Mwakangale

UTIMAMU wa akili husababisha kila binadmu kuzingatia kuishi kulingana na sheria na taratibu zilizowekwa ndani ya jamii.

Afya akili ni kati ya maradhi ambayo yanayoleta changamoto miongoni mwa jamii kutokana na baadhi wenye matatizo hayo huleta madhara kwa wengine.

Kwa siku kadhaa kumekuwa na matukio yakiripotiwa ikiwamo mauaji ya watu yanayotokana na uhusiano wa kimapenzi na ndoa.

Akili ndio inayomuongoza mtu katika na ufahamu kupitia ubongo na hii humtambulisha mtu uwezo, utimamu wake ikiwamo mienendo yake kila siku.

Maradhi ya akili ni miongoni mwa magonjwa yanayowakumba zaidi binadamu, ingawaje yapo ambayo hayahusishi mtu kuchanganyikiwa.

Pia maradhi mengine yatokanayo na afya ya akili kutengemaa, ni pamoja na mtu kuchanganyikiwa au kurukwa na akili.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema kuna matukio kadhaa ya watu kujidhuru na kwamba mtu mmoja hufariki dunia katika kila sekunde 40 kutokana na kujiua.

Kutokana na ukubwa wa tatizo hilo, imetengwa kila Oktoba 10 ya kila mwaka, dunia huadhimisha siku ya afya ya akili, lengo likiwa kukuza uelewa.

Ripoti ya Haki a Binadamu mwaka 2019, Tanzania, iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), katika matukio tofauti ndani ya ripoti hiyo, matukio 14 ni ya ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake kwa mwaka huo, na 12 yalisababishwa na vifo vya wanawake.

Kati ya mauaji 12 ya wanawake hao, nane husababishwa na wivu wa kimapenzi.

Pia, LHRC inasema, zaidi ya wanawake 1,500 barani Afrika huuawa na wenzi wao na familia zao. Zaidi ya asilimia 50 ya wanawake duniani kuuawa na wenzi wao au wanafamilia.

### AFYA YA AKILI NI NINI?

Daktari bingwa wa Afya ya Akili na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, (MNH), Dk. Saidi Kuganda, katika mazungumzo na mwandishi wa makala hii, anasema akili ni ustawi na mwenendo wa binadamu kujikimu mwenyewe.

Anasema pia ni uwezo wa kukabiliana na changamoto na kwamba hasira, wivu ni kati ya dalili za maradhi ya akili ambayo huzaa ukatili.

Hata hivyo, matatizo hayo hayapewi kipaumbele katika jamii au hayazingatiwi.

Anasema afya ya akili ni hali ya ustawi kiakili, kimwili, kiuchumi, kisiasa ikiwamo namna ya kukabiliana na changamoto za maisha ya kila siku.

"Hivi vitu vikitengemaa ndio afya ya akili. Sio kwamba mtu haumwi ndio afya ya akili hapana. Afya ya akili ni ustawi wa vitu hivyo, afya ikitetereka mwenendo unabadilika," anasema Dk. Kuganda.



"Hasira inaweza isiepukike katika maisha yetu ya kila siku, lakini tunadhibiti vipi, hasira ni dalili za maradhi ya akili na visipodhibitiwa vinaleta matokeo hasi," anaongeza.

Anasema maradhi ya akili yamegawanyika katika makundi mawili, ya kwanza ni maradhi madogo yasiyohusisha kuchanganyikiwa akili na kundi la pili ni maradhi ya makubwa yanayohusisha kuchanganyikiwa akili.

Dk. Kuganda, anasema maradhi ya akili yasiyohusisha kuchanganyikiwa ni mengi zaidi yapo kila siku kwa kila binadamu anayaishi, lakini kutokana na uwezo wa kuyakabili hapotezi uwezo wa ufahamu kiakili.

"Mtu akibadili mwenendo wake tunajiuliza yupo sawa kweli? Ndio mana mtu anaweza kumuita mtu fulani kichaa! Kwanini? anasema Dk. Kuganda.

Anaeleza kuwa jamii inapoona mabadiliko ya mtu katika mwenendo wake kitabia usikoendana na mazingira, huanza kumpa mtu majina ambayo humtaja kama karukwa na akili, chizi, mwehu, mwendawazimu, kichaa, kachanganyikiwa kabla ya wataalamu kuthibitisha.

"Mfano mtu hajazoeleka kupita bila nguo na ni mwenzetu, lakini ghafla kaja ofisini bila nguo, binafsi nitajiuliza kwanini hata kabla ya kumuuliza mhusika, hii hali haiendani na mazingira, basi huyo atakuwa ana maradhi ya akili," anaongeza

### MAKUNDI MARADHI YA AKILI

Dk. Kuganda, anaeleza kuwa kundi la maradhi madogo ya akili ni pamoja na walio na dalili kama vile hasira, wivu, wasiwasi, woga, sonona, huzuni pamoja na msongo wa mawazo.

Anaeleza kwamba kati ya dalili hizo hasira ndio yenye matokeo hasi zaidi kwa mhusika na jamii na inaweza kuathiriwa.

Kwamba, hasira ni mihemko na hisia hasi kutokana na mazingira ya binadamu, huleta mkwamo kiakili na kushindwa kupambanua mambo na kinyume cha hasira ni hisia chanya ambazo mtu hufurahishwa na kucheka.

"Mfano katika mahusiano ni vyema kujuana mapema tabia kabla ya kuingia mkataba wa kuwa pamoja muda mrefu. Kufahamu tabia zinazovumilika kabla ya kuweka upendo ndani ya moyo wako," anasema Dk. Kuganda anaongeza....

Mahusiano yana sehemu yake katika moyo, uking'oa ghafla maana yake unaacha kovu au kidonda, hii inaweza kumletea mtu madhara.

Wapo wanaopata maradhi kama kisukari, moyo, presha na hata kupunguza kinga ya mwili, huwezi kukaa na hasira kwa muda wa siku tatu ikakuacha salama.

Anaeleza kuwa muda wa kukaa na hasira kwa binadamu yeyote ambaye akili yake imeshindwa kudhibiti mambo ni jambo la kawaida, ingawaje ikikaa zaidi ya siku tatu hadi wiki, wataalamu huanza kuhoji kutengemaa kwa hilo jambo kiakili.

"Mfano mtu au mtoto anaamua kuzira kula kutokana na mama yake kumgombeza au kakasirishwa na rafiki, jirani, kiongozi wake au aliadhibiwa unaweza kumpa muda wa akili yake kudhibiti jambo hilo ni kawaida kwa kila binadamu anaudhiwa hupata hisia hasi za kukasirika, lakini je, anakuwa na hasira kwa muda gani?," anasema mtaalamu huyo.

Kasha anaongeza "Mtu kakukera tangu jana usiku wa saa tano na hadi asubuhi saa tano bado amekasirika, hajaongea na mtu na si kawaida yake, hayo ni mabadiliko ya mwenendo wake, hii inaweza kuwa dalili ya maradhi ya akili,"

Anabainisha kuwa hasira ina tabia ya kujirudisha nyuma ndani ya ubongo, na akili ikishindwa kujipambanua inamrudia mwenye hasira na kumletea hisia tofauti, na hata mtu kujichukia mwenyewe na kigezo pekee cha maradhi ya akili ni kutotengemaa na mabadiliko yasiyo ya kawaida ikiwamo mienendo.

"Uvumilivu kwa ambao wapo kwenye ndoa, mahusiano ni muhimu kutafuta mikakati ya awali ya kusuluhisha, kuliko kuchukua maamuzi ya hasira huwa na athari hasi ambazo ni mbaya kiafya na kijamii." Anasisitiza

Anafafanua kwamba kinga ya mwili inapopungua kutokana na hasira na kusababisha maradhi ya akili pia inaweza kuwa sababu ya kushambuliwa na maradhi mengine ya mwili.

Anaelezea kuhusu wivu, Dk. Kuganda, anasema kitendo hicho kikipitiliza husussan kwenye mahusiano ni moja ya dalili ya maradhi ya akili yasiyofikia kiwango cha juu cha kuchanganyikiwa.

"Mke, mume au mpenzi wako akitoka kidogo akirudi unaanza kumkagua ni dalili ya maradhi madogo ya akili, kwa hiyo wataalamu wa afya akili tutamsikiliza mtu huyu kwa kuzingatia maelezo yake,"anasema.

### WIZARA YA AFYA

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Waze na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, wiki chache zilizopita aliagiza maofisa ustawi wa jamii katika halmashauri nchini, kutatua, matatizo yaliyopo kwenye familia hasa matukio ya watu kujidhuru ikiwamo kujiua.

Hii ni baada ya matukio kama hayo kutokea nchini, ikiwamo la Desemba 10, mkazi wa Kinondoni, jijini Dar es Salaam, akidaiwa kumkata kwa mapanga mkewe.

Dk. Gwajima. anasema kwamba matukio hayo yamekithiri ikiwamo migogoro kuhusu mgawanyo wa mali.

Anasema tukio la Desemba 10, mkazi wa Kindondoni, ambaye inadaiwa alimtaka mkewe mapanga ni baada ya kumlazimisha awanyweshe sumu watoto wake, ili wafe.

"Vitendo vya kikatili na kunyimwa haki havivumiliki kwenye ardhi ya Tanzania. Tusijiue, tusijidhuru au kuwadhuru wengine kwa sababu ya msongo wa mawazo wakati serikali ipo kwa ajili ya wote wanaoonewa na kunyanyaswa," alisema Dk. Gwajima.

Waziri anasema kuwapo kwa matukio hayo ni kwamba kuna ukatili wa kijinsia katika familia, matatizo ya kisaikolojia ambayo hayapaswi kufumbiwa macho na jamii.

HABARI KIMATAIFA

# Rais wa Malawi asikitika bunge kukataa uteuzi wake

**Lilongwe,** MALAWI

RAIS wa Malawi, Lazarus Chakwera, amesema huku akiongeza juhudi za kupambana na ufisadi, ameona dalili ya kucheleweshwa kwa sababu bunge linakataa kuthibitisha Uchaguzi wake, ikiwamo mkuu wa kuongoza Ofisi ya Kupambana na Rushwa.

Akihutubia bunge wiki hii, Rais Chakwera alisema alisikitishwa na kukatishwa tamaa na kamati kukataa jina la mteule wake, Martha Chizuma, siku moja kabla ya kuhutubia bunge.

Kamati ya Uteuzi wa Umma ya Bunge (PAC), ilisema siku ya Jumanne, kwamba Chizuma alikataliwa kwa sababu alishindwa kupata alama zinazohitajika kwa uthibitisho.

Nusu ya wabunge katika kamati hiyo walimpa alama za chini, baada ya mahojiano ya tathmini na matokeo yaliyokusanywa yalionyesha, Chizuma alipata alama 15 tu kati ya 25 inayowezekana, chini ya kiwango cha chini cha kufaulu ambacho ni alama 17.

Chakwera aliwataka wabunge waweke kando maslahi ya kisiasa na ya kibinafsi na wafanye sehemu yao katika kuharakisha mabadiliko ambayo Wamalawi wanayatafuta.

Tangu alipoingia madarakani mwaka mmoja uliopita, Chakwera ameendesha kampeni ya kupambana na ufisadi ambayo imesababisha watu kadhaa muhimu, pamoja na mshauri wa usalama wa Rais wa zamani, Peter Mutharika, kukamatwa.

Chakwera alisema anaamini uteuzi wa Chizuma, anayejulikana kama iron lady utasukuma mbele lengo hilo.

Chizuma, ambaye kwa sasa ni msimamizi wa masuala ya umma Malawi, aliwaondoa maofisa wakuu watano kwenye nyadhifa zao kwenye kituo cha mdhibiti wa mawasiliano wa Malawi, akisema waliajiriwa kinyume cha sheria wakati wa utawala wa zamani wa Mutharika na chama tawala cha Democratic Progressive Party (DPP).

Mbunge Ashems Christopher Songwe, ambaye ni wa Chama cha Congress cha Malawi cha Chakwera, alisema kwamba kuna madai wabunge wa upinzani walishawishiwa kupita kiasi kumkataa Chizuma.

Ripoti za vyombo vya habari vya Malawi, vilisema moja ya madai ni kwamba wabunge wa upinzani walichukua fedha kutoka kwa wafanyabiashara mafisadi, ili kupiga kura dhidi yake.

Mchambuzi wa kisiasa, Vincent Kondowe, alisema kwa kumkataa Chizuma, wabunge hawajafanya makosa yoyote.

Wakati huo huo, bunge limepitisha hoja inayoelekeza Kamati ya Uteuzi wa Bunge kuwasilisha ripoti ya kina bungeni, ifikapo Jumanne wiki ijayo kueleza kwa nini imemkataa Chizuma.

Wataalam wa sheria walusema ikiwa uamuzi huo utasimama, rais atawasilisha tena jina la Chizuma au atatangaza mteule mpya.

**VOA**



Kijana wa Kipalestina akiendesha mkokoteni uliobeba vitu na mdogo wake wakati wakiyahama makazi yao kufuatia mashambulizi ya angani yanayofanywa na Israel na kusababisha majengo, nyumba kuharibiwa vibaya, mjini Gaza, jana. **(PICHA: REUTERS)**

# Mahakama Kuu Kenya yapinga BBI

**Nairobi,** KENYA

MAHAKAMA Kuu Kenya, imesema kuwa mchakato wa BBI wa kuifanyia mageuzi Katiba ya nchi hiyo, unaongozwa na Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga, ni kinyume cha sheria.

Uamuzi huu wa majaji wa tano wa Mahakama Kuu, umekuja baada ya bunge la kitaifa na lile la Senate, kupitisha muswada unaopendekeza mageuzi hayo maarufu kama BBI, yaliyoanza kutumiwa mwaka 2010.

Majaji hao walisema, Rais Kenyatta alitumia kifungo cha Katiba kuanzisha mchakato huo, badala ya kuanzia kwa wananchi na hivyo kuufanya mchakato huo kuwa kinyume cha sheria.

Rais Kenyatta na kiongozi wa upinzani Odinga wamekuwa wakitetea mchakato huo wa mageuzi ya katiba kwa kile wanachosema mabadiliko hayo yatasaidia kumaliza machafuko ya kila baada ya uchaguzi mkuu.

Miongoni mwa mageuzi hayo ni kuundwa kwa maeneo bunge mapya 70, mawaziri kuwa wabunge na kuundwa kwa wadhifa wa waziri mkuu, manaibu wake wawili na kiongozi wa upinzani.

Naibu Rais William Ruto, ambaye ameonyesha nia ya kuwa rais wa nchi hiyo na kutofautiana na Rais Kenyatta, kuhusu mchakato huo amekuwa katika mstari wa mbele kupinga mageuzi ya Katiba.

Serikali ya Kenya inatarajiwa kukata rufaa, kupinga uamuzi huo wa Mahakama Kuu.

**RFI**

## Marekani yalipa mamilioni ya dola kulikomboa bomba la mafuta

**Washington**, MAREKANI

BOMBA kubwa la mafuta la Marekani, limeripotiwa kuwalipa wahalifu yaani wadukuzi wa mtandao, wanaofahamika kama DarkSide, kiasi cha dola za kimarekani milioni tano, kulikomboa, baada ya bomba hilo kuvamiwa mtandaoni.

Bomba la Colonial lilikuwa linapata wakati mgumu kufanya shughuli zake, baada ya kudukuliwa mwishoni mwa wiki iliyopita na kusababisha kuzimwa kwa huduma za mtandaoni katika bomba hilo kwa muda wa siku tano.

Hali hiyo ilifanya usambazaji wa mafuta kuwa mgumu katika maeneo yote Marekani.

Ripoti kutoka CNN, The New York Times, Bloomberg na The Wall Street Journal all zilisema gharama za kikombozi zililipwa kwa kunukuu vyanzo vyake.

Siku ya Ijumaa, wateja wa teknolojia kubwa ya Japan ya Toshiba, walisema upande wa Ulaya, nchini Ufaransa, wahalifu walishambuliwa na genge hilo hilo la uhalifu wa mtandaoni.

Colonial ilitangaza kurudisha operesheni zake siku ya Jumatano, wiki hii, ingawa ilitoa angalizo kuwa itachukua siku kadhaa, kuanza kusambaza bidhaa na kurudi katika taratibu zake za kawaida.

Usitishwaji wa usambazaji wa mafuta ya dizeli, petroli na mafuta ya ndege katika taifa zima la Marekani, kumesababisha bei za bidhaa hizo kupanda na sheria ya dharura kupitishwa Jumatatu wiki hii ya kutangaza hali ya dharura.

Bomba hilo kwa jina la Colonial, linabeba mapipa milioni 2.5 kila siku, sawa na asilimia 45 ya mahitaji yoye ya mafuta ya Pwani ya Mashariki nchi hiyo na liinasambaza mafuta ya dizeli, petroli na mafuta ya ndege.

Wahalifu wa mtandaoni, walifanya hujuma dhidi ya bomba ambalo limeshindwa kushindwa kufanya kazi tangu siku ya Ijumaa wiki iliyopita na mpaka sasa bado oparesheni ya kujaribu kurudisha huduma za bomba hilo zinaendelea.

Hali ya dharura inaruhusu mafuta kusafirishwa kwa njia ya barabara.

Jumla ya majimbo 18 yamepewa muda kidogo kusafirisha mafuta ya petroli, dizeli na ya ndege na aina nyingine za bidhaa za mafuta.

**VOA**

## Rais Maldives apelekwa Ujerumani kutibiwa baada ya jaribio la kumuu

**Berlin,** UJERUMANI

RAIS wa zamani wa visiwa vya Maldives, Mohamed Nasheed, ambaye alijeruhiwa vibaya kwenye jaribio la kumuuwa mwanzoni mwa mwezi huu, amesafirishwa hadi Ujerumani kwa matibabu. Mwanasiasa huyo mwenye umri wa miaka 53, alishambuliwa kwa bomu la kutegeshwa kwenye pikipiki wiki moja iliyopita katika mji mkuu, Male.

Alifanyiwa operesheni 16, kuondosha vipande cha vyuma kwenye ini lake, mapafu na tumbo.

Juzi, hospitali alikokuwa akitibiwa ilimpa ruhusa na baadaye akapelekwa uwanja wa ndege kwa ajili ya safari ya hadi Ujerumani.

Polisi inawashikilia watu watatu, wanaoshukiwa kuhusika na mashambulizi hayo, ambao wana mafungamano na itikadi kali za kidini.

Nasheed alikomesha miongo kadhaa ya mfumo wa chama kimoja kwa kuchaguliwa rais wa kwanza wa kidemokrasia mwaka 2008, ingawa alipinduliwa mwaka 2012.

**DW**

# Wadau wa mabwawa wasisitizwa sheria

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa mabwawa wamesisitizwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo na kuhakikisha mabwawa yanasajiliwa kwenye mamlaka husika.

Lengo ni kuyafanya yatambulike kisheria kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza kwa jamii na mazingira kwa ujumla.

Wito huo ulitolewa jijini Mwanza na Mkurugenzi Msaidizi Utunzaji wa vyanzo vya maji kutoka Wizara ya Maji, Rosemary Rwebugisa, wakati wa kufunga warsha ya wadau kuhusu miongozo ya usalama wa mabwawa.

"Zingatieni miongozo ya usalama wa mabwawa, tunahitaji uwapo wa mabwawa yenye manufaa na ambayo ni salama kwa viumbe hai na mazingira na si vinginevyo," alielekeza Rwebugisa.

Rwebugisa alisisitiza umuhimu wa kutumia watalam wa mabwawa waliosajiliwa kuanzia hatua za awali za usanifu hadi hatua ya usimamizi wakati tayari yameanza kazi ili kuepukana na changamoto zinazoweza kusababisha madhara.

Alisema baaadhi ya mabwawa hukutana na changamoto kadhaa, huku mengine yakishindwa kukidhi matakwa ya matumizi yaliyokusudiwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya kutoshirikisha wataalamu.

"Kabla hamjaanza kuchimba ama kujenga mabwawa, hakikisheni mnashirikisha wataalamu ili wajiridhishe kulingana na utaalamu wao kama bwawa linalotarajiwa kujengwa mahali hapo linastahili na pia namna gani lijengwe ili kuepukana na changamoto zinazozuilika," alisisitiza Rwebugisa.

Alizitaja baadhi ya changamoto zinazoweza kujitokeza endapo bwawa litajengwa bila ushauri wa kitaalamu ni kuvuja, jambo ambalo alisisitiza kuwa ni hatari kwa afya na maisha ya viumbe wanaozunguka eneo husika.

Alisema jamii pia inapaswa kuelimishwa na kutambua umuhimu wa mabwawa hasa ikizingatiwa kwamba mabwawa yanazo faida lukuki ambazo baadhi yake alizitaja kuwa utunzaji wa mazingira kwa kuhifadhi taka hatarishi lakini pia ni chanzo cha mapato kutegemeana na aina ya bwawa.

Akizungumzia kuhusu warsha, Rwebugisa alisema imejikita kujadili Miongozo ya Usalama wa Mabwawa na kwamba wadau walioshiriki wajitahidi kufuata miongozo walioijadili.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akizungumza na waumini wa dini ya Kiislamu wakati wa swala ya Eid El fitri, katika viwanja vya Bomani, wilayani Pangani, mkoani Tanga jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Muhimbili yawanoa wanafunzi mabadiliko ya mwili

**Na Sabato Kasika**

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Malamba-Mawili, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, wamepewa elimu ihusuyo mabadiliko ya mwili kutokana na ukuaji na madhara ya mimba za utotoni, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani ambayo inafikia kilele chake leo.

Elimu hiyo ilitolewa juzi na wauguzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Upanga na Mloganzila, kwa kushirikisha wanafunzi 1,400, kwa kuwafundisha mada mbalimbali ikiwamo athari za matumizi ya dawa za kulevya.

Wanafunzi hao pia walifundishwa, namna ya kujikinga na mimba za utotoni na kufahamu njia mbalimbali za kujikinga na magonjwa yanayoambukizwa ikiwamo UKIMWI.

Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Hospitali ya Taifa Muhimbili, David Mpayuke, alisema, wametoa elimu hiyo ili kuwahamasisha wanafunzi kujiunga na fani ya uuguzi pamoja na kuboresha afya ya jamii, afya ya akili, afya ya uzazi, usafi na huduma ya kwanza shuleni.

"Uuguzi ni fani inayohitaji wataalamu wengi zaidi ili kuboresha afya ya jamii, hivyo wanafunzi wanahitaji kupata elimu zaidi na kufikia ndoto zao kwa kujifunza namna watakavyokabiliana na magonjwa mbalimbali, kujitunza na kupambana na mazingira yanayowazunguka," alisema Mpayuke. Ofisa Muuguzi Catherine Bigendaku kutoka Muhimbili-Mloganzila ambaue alifundisha wanafunzi hao kuhusu mabadiliko ya mwili, alisema ni muhimu kila mwanafunzi ajue anavyokua.

"Kuna madhara mengi yanayotokana na ukuaji ambayo wakati mwingine husababisha mimba za utotoni, hivyo tumeona tutumie maadhimisho ya siku hii kukaa na wanafunzi hawa ili kuwaelimisha," alisema Catherine. Akizungumza kwa niaba ya walimu wa shule hiyo, mwalimu Daniel Mfanga aliwashukuru wauguzi hao kwa elimu walioitoa na kusema itawasaidia wanafunzi kujua na kukabiliana na changamoto mbalimbali za afya.

"Vilevile watakuwa mabalozi wazuri watakaporudi nyumbani kwao ili kueneza elimu walioipata na hatimaye kusaidia kupunguza au kumaliza tatizo la mimba ambalo limekuwa likiwaandama," alisema mwalimu Mfanga.

Maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani, hufanyika Mei 12 ya kila mwaka, ambapo mwaka huu kitaifa yalifanyika mkoani Manyara yakiwa na kaulimbiu ya "Wauguzi sauti inayoongoza, Dira ya huduma ya afya".

# NMB yawapa chakula watoto yatima Pemba

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

BENKI ya NMB tawi la Pemba, imekabidhi vyakula vyenye thamani ya Sh. 700,000 kwa watoto yatima Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Akikabidhi vyakula hivyo vikiwamo mchele, sukari, mafuta ya kula pamoja na unga wa ngano, Meneja wa NMB tawi la Pemba, Hamad Msafiri, alieleza kuwa lengo la msaada huo ni kuwasaidia watoto hao katika kipindi hichi cha sikukuu ya Eid el Fitri.

Msafiri alieleza kuwa NMB imekuwa ikifanya kazi nyingi ikiwamo kusaidia jamii kwa kutoa vifaa na mambo mbalimbali ambayo ni muhimu kwa jamii.

Meneja huyo alisema kwa vile kipindi hichi ni cha mwisho wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, NMB iliona ni vyema kuwafikia watoto hao ambao wana uhitaji maalum ili kuwapatia chochote ambacho kitawasaidia katika kipindi cha sikukuu.

"Wito wangu kwa taasisi nyingine pamoja na jamii kuendelea kusaidia na kuona kuna umuhimu mkubwa wa kuwasaidia ambao mana mahitaji maalum," alieleza Msafiri.

Akitoa neno la shukrani kwa uongozi wa NMB, mwanafunzi Shaame Chapa Hamad, aliushukuru uongozi huo kwa msaada waliowapatia na kueleza kuwa itakuwa chachu ya kukiendeleza kituo chao.

Aidha Shaame aliyataka mashirika mengine pamoja na wananchi waone ipo haja kuwapo kwa kituo hicho cha kulelea yatima, hivyo ni wajibu wao kuungana na NMB katika kukiendeleza mbele kituo hicho, kwani kina faida kwa watoto hao.

Mlezi wa kituo hicho, Khamis Mbwana Haji, aliupongeza uongozi wa NMB kwa kuwajali watoto hao na kueleza kuwa sababu za kwenda katika kituo na kuwapatia msaada, ni jambo la faraja sana.

**"Wito wangu kwa taasisi nyingine pamoja na jamii kuendelea kusaidia na kuona kuna umuhimu mkubwa wa kuwasaidia ambao mana mahitaji maalum," alieleza Msafiri.**

# HADITHI

# Aolewe au afe-6

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.
Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho.
Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini.
Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

Mama yake alishtuka na kushangaa kwa wakati mmoja.

"Nini wewe?"

Hakujibiwa.

"Nyoka?"

Bishada alifungua fundo kwenye khanga na kumpa mama yake karatasi ile.

"Bishada Binti Ngoma. Uzuri wako usifanye fimbo ya kutupigia sisi wanaume. Najua baada ya ule mkutano utakubali moja ya barua zitakazokuja. Naitwa mzee Buntungwa, nadhani unanifahamu. Kesho tunatuma mshenga kwa ajili ya kijana wangu Limiko. Hiyo ndiyo uikubali. Vinginevyo unajitafutia matatizo. Kwa hiyo una mawili tu ya kuchagua. Ukubali barua ya kijana wangu Limoko ili uishi. Au ukatae ufe. Ndiyo utakufa na najua mimi mbinu nitakayotumia ili kukuondoa hapa duniani. Kumbuka kuwa hata ukimkubali mtu yoyote na kumkataa Limiko, kifo ni halali yako. Na kwa sababu kijiji kimeshawachoka wewe na familia yako, huwezi kwenda kushtaki popote juu ya kutishia ukasikilizwa. Uamuazi sasa unao mwenyewe, ahsante."

Mama hakuamini alichokuwa akikisoma. Bishada aliingia chumbani kwake na akuanza kuangua kilio.

Akili yake moja kwa moja ikamtuma kuwa kilichobaki wahame tu kijiji hicho. Watoke hapo waende wakajiandikishe kwenye kijiji chochote cha mbali. Huku watakachobakisha ni ardhi yao na mashamba tu. Hali hiyo ilishaanza kumchosha. Ni kweli alikuwa akigombana mara kwa mara na binti yake juu ya kutotaka kuolewa. Lakini hii ya kulazimisha na kutaka kumuua Bishada ilimfikirisha na kumtisha. Aliona kabisa kilichobaki wanamuulia tu binti yake ili wakose wote. Hakuonekana ana dalili za kumkubali mwanaume yoyote yule.

Kabla ya uamuzi wote huo ambao ulikuwa unamsubiria mzee Ngoma arejee aliingia chumbani kwa binti yake na kumkuta machozi yalimtoka akiwa amejikunyata.

"Mama, kwani kuolewa ni lazima au hiari?" Aliuliza kwa uchungu.

"Hiari mwanangu." Alijibu kwa uangalifu.




"Sasa mbona mimi nalazimishwa. Huyu anataka eti nimkubali kijana wake Limiko. Hata kama nikikubali kwa sababu ya kuogopa kuuawa, itakuwa ni ndoa au utumwa?" Alihoji Bishada kwa hasira kana kwamba mama yake ndiyo anayemlazimisha.

*********************************

Wiki ya pili sasa ilielekea kukatika. Zilibaki wiki mbili na kitu hivi ili ufikie mwezi mmoja ambao umetolewa na mwenyekiti wa kijiji wa familia ya mzee Ngoma kuendelea kubaki kijiji cha Mtakuja au kuondoka.

Kilichotakiwa kufanywa ni kwamba baada ya mwezi kwisha, angalau tu barua moja iwe imekubaliwa.

Barua za posa ziliendelea kumiminika. Lakini zilikaa tu kama ziko posta, zinasubiri wenyewe waje kuzichukua.

Kali kuliko yote ni kwamba kuna barua, karatasi au vipeperushi vya vitisho ambavyo vilikuwa vinatupwa mlangoni kwa kina Bishada.

Asubuhi wakiamka wanakuta vikaratasi hivyo. Vilifanana na kile ambacho alikiokota Biashada wakati anakwenda kisimani. Vyote vilikuwa na lengo moja tu. Kumtisha Bishada. Kuitisha familia. Kila kijana. Kila mwanaume. Kila mzazi wa kijana alitaka kijana wake ndiyo akbaliwe. Vinginevyo yatatokea maafa. Bishada atauawa. Sasa wachague. Aolewe au afe. Wengine walitishia kumuua kwa sumu. Wengine kwa silaha. Wapo waliotishia kuondoa uhai wake kwa uchawi.

Baada mkwara wa kijiji, waposaji wengi walijua kuwa sasa Bishada atakubali. Lakini kila mmoja alitaka yeye ndiye akubaliwe.

"Sasa kama hata akimkubali mmoja, waliobaki si watamdhuru binti yangu?" Alijiunza mama Bishada.

Ni swali ambalo pia mzee Ngoma, baba Bishada alikuwa anajiuliza.

Mtu na mkewe waliona kabisa hakuna uwezekano wa kuendelea kuishi kwenye kijiji hicho.

Kwa upande wa Bishada, pamoja na kujua kuwa sasa hata akimkubali mmoja bado atakuwa kwenye matatizo, lakini msimamo wake uliendelea kuwa ule ule kuwa bado hakuwa tayari kuolewa.

Pamoja na kuishi maisha ya tabu, akijua maisha yake yako hatarini, lakini Bishada bado aliendelea na maisha yake ya kawaida.

Siku hiyo alikuwa kisimani peke yake akichota maji. Alipomaliza alichukua ngata tayari kuiweka kichwani.

Ghafla ndoo ilisukumwa ikaanguka. Maji yakamwagika. Aligeuka na kukutana na sura ya kijana mmoja ambaye alishawahi kumtongoza akamkataa.

"Leo ndiyo utanijua kama mimi ni nani."

"Deo mimi sitaki."

"Hapa hakuna mtu yoyote anayetuona. Unaliona hili panga?." Alisema huku akitoa panga kukuu lenye kutu.

"Nyamaza wewe, sivyo nitakuua na hakuna mtu yoyote atanifunga. Kijiji kimeshawachoka. Ndiyo kwanza watafurahi wewe kufa. Watu watafanya sherehe na kunipongeza. Hakuna anayekutaka wewe hapa kijijini. Umewakwanza wengi sana."

Bishada alitetemeka. Hakujua la kufanya. Alijua akipanua domo lake tu, basi panga lile butu litaishia mwilini. Hakujua afanye nini. Kukimbia itakuwa ni kujidanganya. Alijua asingeweza kufika hata hatua ishirini kabla ya kukamatwa na hiyo ingekuwa hatari zaidi kwake.

Alichokuwa anaombea hapo kutokee mtu yoyote ambaye anakuja kisimani. Haikuwa hivyo Hakukuwa na dalili yoyote ya mtu.

Deo kijana wa kijiji hapo alimkamata mkono kwa nguvu, huku uliobaki ukiwa ameshika panga.

"Nifuate huku." Kitendo kilifuatiwa na maneno.

Bishada alipelekwa sehemu ambayo si njia ya kwenda nyumbani au kurudi. Bali walikatisha kuelekea porini. Sehemu ambayo watu hawapiti.

Deo aliporidhika na sehemu ila alisimama na kumuachia mkono.

"Sasa ili nisikudhuru au kukumaliza, vua nguo mwenyewe. Nimekutongoza sana, unajifanya bonge la mrembo, kila mtu hapa kijijini umemkataa. Hata kuolewa unakataa. Sasa leo umepatikana."

"Sitaki."

"Weee, nimekwambiaje? Nitakutia panga wewe." Akasema huku akiinua panga lake juu kumtishia.

"Basi navua." Bishada alisema huku akiteteka. Kabla hajajua nini cha kufanya alipigwa vibao viwili vya nguvu ambavyo vilimvuruga kabisa.

"Fanya haraka."

Hakuwa na jinsi. Alitekeleza maagizo ili mradi tu asimdhuru au kumuua.

"Ukifanya ninavyotaka nitakuachia, ila usimwambia mtu." Deo alisitiza.

Deo alipagawishwa na mwili mororo wa msichana huyo. Alikuwa anaona tu sura yake na urembo, lakini hakuwahi kuona mwili wake.

Udenda ulimtoka. Wakati Bishada alitoa nguo zake moja baada ya nyingine. Deo naye alianza kuchojoa suruali yake.

"Mtoto mzuri kama wewe, unakataa wanaume kaka sisi."

Mate yalimtoka Deo. macho yake yalikuwa yakiendelea kupagawishwa na Bishada.

Akili ikampaa. Sasa kazi iliyokuwa imebaki ni moja tu. Kabla hajafanya chochote kile alishtukia akirushwa hapo alipo na kudondokea mbali, baada ya kupigwa na kitu kizito kwenye taya.

"Unataka kufanya nini hapo?"

*Itaendelea Jumamosi*

## HABARI MICHEZO

# MADRID
## KUPAMBANA HADI DAKIKA YA MWISHO LALIGA



**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema kikosi chake kitapambana hadi dakika ya mwisho kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada juzi Alhamisi kupunguza pengo la pointi hadi mbili dhidi ya vinara, Atletico Madrid.

Madrid walishinda mabao 4-1 nyumbani kwa Granada na kuongeza presha kwa vinara hao zikiwa zimebaki mechi mbili ligi kufikia mwisho, huku wakipanda nafasi ya pili na kuwaacha Barcelona nafasi ya tatu baada ya mwanzoni mwa wiki hii kutoka sare ya 3-3 na Levante.

Atletico wamebakia kileleni mwa msimamo wakiwa na nafasi kubwa ya kutwaa taji lao la kwanza la LaLiga tangu msimu wa 2013-14, lakini kikosi hicho cha Zidane bado kinaliwinda kwa karibu.

"Tutaendelea kupambana; kuna mechi mbili zimebaki na tutakwenda hadi mwisho, hadi dakika ya mwisho, tunajitoa kwa kila kitu," alisema Zidane mara baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

Mechi mbili za mwisho za Atletico ni nyumbani dhidi ya Osasuna waliooko nafasi ya 11 na ya pili ni ya ugenini dhidi ya Valladolid walioko nafasi ya 18.

Huku Real wenyewe wakibakiza ugenini dhidi ya Athletic Bilbao waliko nafasi ya tisa na nyumbani dhidi ya Villarreal walipo nafasi ya saba.

Zidane alifurahishwa na ushindi dhidi ya Granada kwani kumewarudisha kwenye mbio za ubingwa.

"Ni suala la kuhusu mabao," alisema Mfaransa huyo. Tulicheza vizuri, tulilinda vizuri pia."

## LAMPARD KUMRITHI HUDGSON PALACE

**LONDON, England**

FRANK Lampard yupo kwenye orodha ya majina yanayotajwa kurithi mikoba ya Roy Hodgson pale Crystal Palace.

Lampard, ambaye ni mchezaji na kocha wa zamani wa Chelsea, hakuwa na wakati mzuri sana kule Stamford Bridge ambapo alitimuliwa kwenye msimu wake wa kwanza na nafasi yake ikachukuliwa na Thomas Tuchel.

Lampard anaweza kupata kazi hiyo endapo tu, Crystal Palace wataamua kumuacha kocha wao Hodgson aondoke klabuni hapo mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Kwa mujibu wa Telegraph, orodha ya majina yaliyotolewa, jina la Lampard limeonekana kupewa kipaumbele kuchukua nafasi hiyo.

Ingawa kuna majina mengine kama kocha wa Burnley, Sean Dyche na kocha wa zamani wa Bournemouth, Eddie Howe, ambaye anahusishwa kujiunga na Celtic kwa muda sasa.

Endapo Lampard atafanikiwa kuchukua mikoba hiyo pale Crystal Palace, basi anaweza kufanya sajili kadhaa kuimarisha kikosi chake.

Miongoni mwa wachezaji hao ni Tammy Abraham, ambaye anatarajiwa kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

Frank alikalia kiti cha ukocha wa Chelsea kwa muda wa miezi 18 tu.

## MBAYA WA GUARDIOLA KUCHEZESHA FAINALI UEFA

**NYON, Uswisi**

SHIRIKISHO la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa), limemtangaza Antonio Mateu Lahoz, kuwa mwamuzi atakayechezesha mchezo wa fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya kati ya Manchester City na Chelsea, Mei 29, mwaka huu.

Mateu raia wa Hispania mwenye umri wa miaka 44, anakumbukwa kama mbaya wa kocha wa Man City, Pep Guardiola ambaye aliwahi kumtoa nje kwa kadi nyekundu.

Mwamuzi huyo alitoa kadi nyekundu baada ya Guardiola kumlalamikia bao wakati wa mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool mwaka 2018.

City walishinda kwa bao 1-0 wakati huo wakijaribu kupindua matokeo ya 3-0 waliyoyapata katika mchezo wa kwanza.

Pia mwaka 2017 kwe michuano hiyo, alishindwa kutoa adhabu kwa faulo ya kipa wa Monaco, Danijel Subasic dhidi ya Sergio Aguero.

Subasic alipaswa pia kutolewa nje kwa kadi nyekundu, lakini Aguero ndiye alionyeshwa kadi ya njano kwa kudaiwa kujidondosha.

Ingawa City ilishinda kwa mabao 5-3 baada ya Radamel Falcao kupata penalti yenye utata iliyookolewa na Willy Caballero, walitolewa kwa mabao ya ugenini kutokana na kupoteza mchezo wa pili.

Oktoba 2017, Mateu alitoa penalti mbili kwa Napoli wakati wa ushindi kwa vijana wa Guardiola wa 2-1 dhidi ya Waitaliano pale katika mashindano hayo.

Mateu pia ana rekodi ya kuchezesha mechi mbili za Chelsea kwenye michuano hiyo. Alicheza mwaka 2014 wakati Blues ikishinda bao 1-0 dhidi ya Sporting Lisbon na 2015 wakati Chelsea wakipoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Porto.

HABARI MICHEZO



# MARTINEZ

## AWANIWA LIVERPOOL, MAN CITY

**LIBERPOOL, Egland**

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Lautaro Martinez, anawaniwa na klabu mbili za Ligi Kuu England, Manchester City na Liverpool, kwa mujibu wa 90min.com.

Kwa mujibu wa ripoti, Inter ipo tayari kuwauza nyota wake akiwamo Martinez kwa sababu ya kujinasua na hali mbaya ya kifedha inayoikabili timu hiyo, ambayo imetwaa taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu huu kwa mara ya kwanza baada ya miaka 10.

Ingawa Inter imeweka dau la pauni millioni 100, lakini imedaiwa inaweza kushuka hadi angalau mpaka pauni milioni 70.

Raia huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 23, kwa muda mrefu alikuwa anawaniwa na Barcelona.

Lakini kutokana na hali mbaya ya kiuchumi inayoikabili Barcelona, uwezekano wa kumsajili nyota huyo unaonekana kuwa mgumu kwa sasa.

Martinez amecheza mechi 36 na Inter, huku akiwa amefunga mabao 16 na kutoa pasi za mwisho nane.

Man City wanahitaji saini ya mshambuliaji huyo ili awe mrithi wa Sergio Aguero, ambaye atatimka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu.

## XAVI AONGEZEWA MIAKA MIWILI AL-SADD

**DOHA, Qatari**

XAVI Hernandez amekubali kuongeza muda wake wa kukaa katika kikosi cha Al-Sadd cha Qatar kwa miaka mingine miwili, klabu yake imethibitisha.

Kukubali kwa Xavi kuendelea kuinoa klabu hiyo, maana yake sasa kumepunguza uvumi kwamba, angeweza kutua katika klabu yake ya zamani ya Barcelona kwa msimu ujao.

Kiungo huyo wa kati wa zamani alijiunga na Al-Sadd kama mchezaji mwaka 2015 baada ya miaka 17 ya kubeba mataji na Barca, na sasa ni kocha mkuu baada ya kutundika daluga mwaka 2019.

Mwezi uliopita aliongoza timu hiyo kutwaa taji la ligi ya ndani ya Qatar huku akiwa bado hajapoteza mchezo.

Xavi alikataa nafasi ya kuwafundisha miamba wa Catalunya Januari 2020 baada ya Ernesto Valverde kufungashiwa virago na ameendelea kuhusishwa na kwenda huko Camp Nou, hata tangu Ronald Koeman alipochukua nafasi ya Quique Setien Agosti mwaka jana.

Hatima ya Koeman pale Barca bado imegubikwa na sintofahamu baada ya kuwa na msimu mgumu.

Na kwa sababu ya makubaliano mapya ya Xavi na Al-Sadd inamaanisha kuwa raia huyo wa Uholanzi anaweza asiwe na wasiwasi juu ya kiungo huyo wa zamani wa Hispania kuchukua nafasi yake hivi karibuni.

## VALENCIA ATUNDIKA RASMI DALUGA

**QUITO, Uruguay**




NAHODHA wa zamani wa Manchester United, Antonio Valencia, ameamua kutundika daluga na kuachana na mchezo wa soka kama mchezaji.

Valencia alisajiliwa na United akitokea Wigan Athletic mwaka 2009 na alifanikiwa kubeba mataji mawili ya Ligi Kuu England (EPL), Kombe la FA, mataji mawili ya Carabao, Ngao ya Jamii mara tatu na Kombe Ligi ya Europa wakati alipokuwa hapo Old Trafford.

Licha ya kubeba makombe, Valencia alitwaa tuzo mbalimbali ikiwamo ya mchezaji bora wa msimu, bao bora la msimu na mchezaji bora wa msimu aliyechaguliwa na wachezaji wenzake katika msimu wa 2011/12 na 2016/17.

Safari ya unahodha wa United ilianza kwenye mchezo wa fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Ajax mwaka 2017.

Baada ya mchezo huo, Valencia alikabidhiwa rasmi kitambaa cha unahodha wa Man United akichukua mikoba ya Wayne Rooney aliyeondoka hapo Old Trafford.

Mei 12, mwaka 2019, Valencia aliondoka United akiwa ameitumikia klabu hiyo kwa michezo 339 na kupachika mabao 29.

Alirejea nyumbani kwao (Equador) kukipiga katika Klabu ya LDU Quito kabla ya kujiunga na klabu ya Queretaro ya nchini Mexico ambapo amestaafia huko.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER: SAFU YA ULINZI MAN UNITED NI MBOVU

Mabao tuliyofungwa yanakatisha tamaa, hii ni mara ya tatu mfululizo, tunatakiwa kuangalia namna ya...

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amekiri kuna tatizo kwenye safu ya ulinzi ya Manchester United baada ya kufungwa nyumbani mabao 4-2 na Liverpool, juzi Alhamisi usiku.

'Mashetani Wekundu' hao walianza kuongoza kwa bao la Bruno Fernandes, lakini wakajikuta wakikubali kichapo hicho kwenye dimba la Old Trafford mbele ya kikosi cha Jurgen Klopp ambacho kimeongeza matumaini ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Liverpool walisawazisha kupitia Diogo Jota kwa kona ya Nat Phillips, na wakapata uongozi dakika za majeruhi ya kipindi cha kwanza wakati Roberto Firmino alipofunga kwa kichwa kuunganisha mpira wa adhabu ndogo uliopigwa na Trent Alexander-Arnold.

Firmino akafunga bao lake la pili na la tatu kwa Liverpool baada ya kipindi cha pili kwa kuuwahi mpira uliotemwa na kipa Dean Henderson na United wakapata la pili kupitia Marcus Rashford, kabla ya Mohamed Salah kufunga la nne.

Safu ya ulinzi ya United ilionekana kutokuwa fiti huku ikiwa bila nahodha wake, Harry Maguire na hicho kilikuwa kipigo cha tatu mfululizo kwenye mechi nane za mashindano yote.

Pia wameruhusu mabao 27 kufungwa nyumbani kwenye ligi msimu huu, yakiwa mengi zaidi kwa msimu mmoja tangu msimu wa 1969-70.

Na kocha Solskjaer akaonyesha wasiwasi wake namna wachezaji wake walivyocheza dhidi ya Liverpool, lakini akainyooshea zaidi kidole safu yake ya ulinzi.

"Mabao tuliyofungwa yanakatisha tamaa," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Hicho ndicho tunachotakiwa kukifanyia kazi, kwa sababu tumeruhusu kufungwa mabao mengi sana kwa sasa.

"Hii ni mara ya tatu mfululizo, tunatakiwa kuangalia namna ya kuboresha safu ya ulinzi, waliwapa presha wao, lakini ulinzi wetu haukuwa mzuri na ndio maana wakatufunga kirahisi."

## KWA UFUPI

**SIMEONE AMTAKA KEITA**

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, anatajwa kuwa shabiki mkubwa wa kiungo wa Liverpool, Naby Keita mwenye umri wa miaka 26, na anapenda kumuongeza mchezaji huyo wa kimataifa wa Guinea katika kikosi chake. ***(Fichajes via Star)***

**BERTRAND AWANIWA LEICESTER**

LEICESTER City wanavutiwa kumsajili mlinzi wa kushoto wa Southampton, Ryan Bertrand mwenye umri wa miaka 31, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, baada ya kuwatumikia 'watakatifu' hao kwa miaka saba. ***(Leicester Mercury)***

**UPAMECANO AJITAJA UNITED**

MLINZI wa kati wa RB Leipzig, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 22, ambaye atajiunga na mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich baada ya ligi kumalizika, amesema alikata nafasi ya kusajiliwa na Manchester United alipokuwa na umri wa miaka 17. ***(The Athletic)***

**DE PAUL AGOMBEWA**

LEEDS United inaongoza dhidi ya AC Milan katika mbio za kumsajili kiungo, Rodrigo De Paul mwenye umri wa miaka 26 kutoka Udinese, lakini Liverpool pia nao wanavutiwa na raia huyo wa Argentina. ***(Mail)***

**WRIGHT HAMTAKI CEBALLOS**

MCHAMBUZI na mshambuliaji wa zamani wa Arsenal, Ian Wright, haamini kama 'Washikabunduki' hao wanapaswa kumsajili kwa mkataba wa kudumu, Dani Ceballos mwenye umri wa miaka 24, ambaye anacheza kwa mkopo akitokea Real Madrid. ***(Metro)***

**MOURINHO AMTAKA PATRICIO**

GOLIKIPA wa Wolves, Rui Patricio mwenye umri wa miaka 33, ambaye amebakiza zaidi ya miezi 12 kwenye mkataba wake wa sasa, anaweza kuwa mlengwa mkuu wa kocha mpya wa AS Roma, Jose Mourinho.***(Calciomercato)***

**LAPORTA APATA PIGO BARCA**

KIUNGO wa zamani wa Barcelona, Xavi Harnandez, amesaini mkataba mpya wa kuendelea kuifundisha klabu ya Al-Sadd ya Qatar hadi 2023. Kuongeza mkataba kwa Xavi ni pigo kwa Rais wa Barca, Joan Laporta, ambaye anatafuta kocha wa kuchukua nafasi ya bosi wa sasa, Ronald Koeman. ***(Il Milanista)***

**RONALDO KURUDI NYUMBANI**

MAMA mzazi wa Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, Dolores Aveiro, angependa mtoto wake huyo arejee katika klabu ya Sporting Lisbon ya Ureno kama ataondoka Juventus mwishoni mwa msimu huu. ***(Guardian)***

**MARTINEZ HAJASAINI MKATABA**

STRAIKA wa Argentina, Lautaro Martinez, mwenye umri wa miaka 23, bado hajasaini mkataba mpya na Inter Milan wakati akiwa anasubiri kuona mpango mpya wa baadaye wa klabu hiyo, amesema wakala wake. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

**SPURS WAMTAKA ANDERSON**

KLABU ya Tottenham Hotspur ina matumaini ya kumshawishi beki, Joachim Andersen mwenye umri wa miaka 24, kujiunga nao. Msimu huu amekitumikia kikosi cha Fulham akitokea Lyon ya Ufaransa. ***(BT via TeamTalk)***

**LLORENTE APEWA OFA**

MANCHESTER United inaanda dau la pauni milioni 68 kwa ajili ya kiungo Marcos Llorente wa Atletico Madrid, huku Atletico wenyewe wakitaka kuharakisha mchakato wa kumsainisha mkataba mpya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Mirror)***

## HABARI MICHEZO

# MANULA NDIYE KIPA BORA ZAIDI TANZANIA - MBRAZIL

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikishuka katika Uwanja wa FNB maarufu Soccer City ama 'The Calabash', nchini Afrika Kusini kuwavaa wenyeji wao, Kaizer Chief, kwenye mechi ya robo fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha wa Makipa wa mabingwa hao wa Tanzania, Mbrazil Milton Nienov, amesema ubora wa mlinda mlango Aishi Manula kwa sasa haukamatiki nchini.

Simba ambayo inapewa nafasi kubwa ya kusonga mbele katika michuano hiyo, itakuwa na kibarua kigumu leo ugenini hasa kutokana na wapinzani wao, Kaizer Chiefs nao kupenda kucheza kwa kumiliki mpira zaidi, lakini wakiwa na sifa ya kasi.

Akizungumzia mchezo huo, Nienov, ambaye analifahamu vema soka la Afrika Kusini kutokana na kufanya kazi nchini humo kwa muda mrefu, alisema anawajua wachezaji wengi wa Kaizer Chiefs na watakachoweza kukifanya katika mechi hiyo kwa kuwa ni timu kubwa ingawa haifanyi vizuri ligi ya ndani ila Ligi ya Mabingwa Afrika ni kitu tofauti.

"Huwezi kuchukulia poa timu kubwa kama Kaizer Chiefs yenye mashabiki wengi, historia kubwa eti kwa sababu inafanya vibaya kwenye ligi, robo fainali ni kitu kingine tunapaswa kufanya maandalizi makubwa na ninaamini tunakwenda nusu fainali japo si rahisi," alisema.

Kuhusu ubora wa Manula kwa sasa, alisema kabla ya kuja hapa alipatwa na virusi vya corona akiwa nyumbani kwao Brazil na kukaa kwa muda wa wiki mbili, lakini aliomba kutumiwa taarifa zote za makipa haswa Manula kwa sababu ndiye alikuwa anadaka sana.

"Nilikuja nikijua matatizo ya Manula, hivyo nilichokifanya ni kutumia uzoefu wangu wa miaka 20 na tatizo la Manula lilikuwa ni kucheza krosi, mipira ya adhabu na kufungwa mabao ya mbali, lakini sasa nimelimaliza na yupo vizuri na si Manuala tu bali makipa wote, Kakolanya [Beno] na Ali [Salum].

"Kwa hiki kipindi, Manula ni kipa bora zaidi hakuna kipa wa kuweza kusogelea ubora wake hapa nchini, sioni kipa yoyote wa kuweza kumzidi na si kwa sababu mimi ni kocha wake, hapana kwangu mimi hakuna kipa kama yeye hata kwa timu ya taifa yupo mbali sana," alisema Nienov.

**MAANDALIZI...**



Wachezaji wa timu ya KMC FC, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi, kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC utakaopigwa leo katika Uwanja wa Chamazi, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga kwa Namungo leo bila Ninja, Carlinhos

**Na Mwandishi Wetu**

YANGA itashuka dimbani leo katika Uwanja wa Majaliwa, kuivaa Namungo FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara bila nyota wake muhimu wa kikosi cha kwanza.

Katika mchezo huo utakaopigwa majira saa 10:00 alasiri, nyota ambao Yanga inatarajia kuwakosa kutokana na sababu mbalimbali ni pamoja na beki wa kati, Abdallah Shaibu, 'Ninja' na kiungo Carlos Carlinhos.

Katika mchezo huo Kocha Mkuu wa Yanga, Nassredine Nabi, huenda kwenye safu ya ulinzi sasa akalazimika kumwanzisha Dickson Job na Bakari Mwamnyeto, kutokana na Ninja kuwa nje akiuguza majeraha ya misuli, tatizo ambalo linamtesa pia Carlinhos.

Ninja amekuwa kwenye ubora wake kwenye mechi za hivi karibuni jambo ambalo limemfanya kuwa chaguo la kwanza la Kocha huyo raia wa Tunisia, Nabi.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, wachezaji hao wanaendelea na matibabu ili waweze kurejea kwenye ubora wao.

Yanga ambayo ipo katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 57, nne nyuma ya vinara Simba waliopo mechi mbili nyuma, itahitaji kushinda ili kupunguza wigo huo wa pointi, lakini haitakuwa rahisi hasa kutokana na ubora wa Namungo katika mechi zake za hivi karibuni licha ya kuwa katika nafasi ya 10 ikiwa na alama 35 zilizotokana na kushuka dimbani mara 25.

Katika mechi ya raundi ya kwanza iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.

# Mbeya City yatoa siri kushinda nne mfululizo

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 2-0 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, juzi Alhamisi, umeifanya timu ya Mbeya City kushinda mechi ya nne mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa kwenye operesheni kabambe kuhakikisha inabaki Ligi Kuu.

Yalikuwa ni mabao ya David Mwasa na Juma Luzio yaliyoifanya timu hiyo kuweka rekodi hiyo, huku ikipaa hadi nafasi ya 11, ikiwa imefikisha pointi 33 kwa michezo 29 ambayo imecheza.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Vicent Msolla, amesema ushindi huo wa nne mfululizo umetokana na ushirikiano wa viongozi, makocha na wachezaji, kwani baada ya matokeo mabovu walikaa na wachezaji kuangalia tatizo liko wapi na kulirekebisha.

"Tumefanyia kazi upungufu wote ambao ulikuwapo awali. Wachezaji nao tulikaa nao tukawasikiliza na wao tukawataka wabadilike, ndiyo maana unaona matokeo haya chanya tunayoyapata," alisema mwenyekiti huyo.

Hata hivyo, alisema wamepata funzo kubwa kuwa ukitaka kufanya vema kwenye ligi hii ni lazima uwekeze pesa.

"Tumejifunza kuwa kwenye Ligi ya Tanzania na mpira wetu ni lazima uwekeze pesa ili kupata wachezaji wazuri na wenye uwezo mkubwa, kwa hiyo msimu ujao tutegemee mabadiliko," alisema mwenyekiti huyo.

Mara ya mwisho Mbeya City kupoteza mechi ilikuwa ni Aprili 15 ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Ihefu kwenye Uwanja wa Sokoine.

Baada ya hapo ilishinda ugenini bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania, ikaichapa Namungo 1-0 ugenini, kabla ya kuipiga JKT Tanzania kipigo cha paka mwizi cha mabao 6-1 nyumbani na baada ya hapo Ruvu Shooting nayo ikafuata kwa kupata kipigo hicho.

Michezo
Jumamosi Mei 15, 2021
Nipashe



SOLSKJAER: SAFU YA ULINZI MAN UNITED NI MBOVU HABARI UK 22

MUDA UTAONGEA...



Winga wa Simba, Luis Miquissone, akiwa mazoezini Afrika Kusini na kikosi cha timu, ambacho leo kitashuka katika Uwanja wa FNB nchini humo kuwavaa wenyeji wao, Kaizer Chiefs, kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA**

## NABI AMALIZA KAZI KWA NAMUNGO LEO

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwasili salama Ruangwa mkoani Lindi, kikosi cha Yanga chini ya Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, amesisitizia wachezaji wake kupambana kutafuta pointi tatu katika mechi yao dhidi ya Namungo FC, itakayopigwa Uwanja wa Majaliwa mkoani hapo leo.

Yanga itashuka dimbani leo ikifahamu ugumu wa kupata matokeo dhidi ya Namungo FC, kutokana na misimu miwili timu hizo kushindwa kutambiana na zimekuwa zikiambulia sare kila zinapokutana, na tayari mzunguko wa kwanza zilitoka sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Benjamini Mkapa.

Lakini Nabi amesema wachezaji wake wako fiti na tayari kwa ajili ya mchezo huo na amemaliza kazi na kuwapa majukumu wachezaji wake na anaamini watahakikisha wanapambana kutafuta alama tatu.

Naye kocha wa Namungo FC, Hemed Morocco alisema: "Mechi itakuwa ngumu kwa pande zote, kwetu tunahitaji kupata pointi tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuendelea kubaki Ligi Kuu, huku wenzetu wakipambana kutafuta nafasi za juu ikiwamo ubingwa wa ligi," alisema Morocco.

# SIMBA, KAIZER NI MTIFUANO

## ●●● Gomes anusa hali ya hatari, atoa tahadhari kwa wachezaji, lakini asema...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, leo wakishuka katika Uwanja wa FNB maarufu Soccer City ama 'The Calabash', ugenini Afrika Kusini kuivaa Kaizer Chiefs katika mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tayari benchi la ufundi la timu hiyo, likiongozwa na Mfaransa Didier Gomes, limenusa hatari.

Leo majira ya saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki, Simba itakuwa inapeperusha bendera ya nchi, itakapocheza mechi ya robo fainali kwenye Uwanja wa FNB ikiwa na kazi moja tu ya kuweka matumaini ya kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza baada ya miaka 47.

Mara ya mwisho Simba kutinga hatua hiyo ilikuwa mwaka 1974 ilipoifunga Heats of Oak ya Ghana ugenini mabao 2-1 na kutoka suluhu nyumbani nchini Tanzania, lakini ikatolewa kwenye hatua ya nusu fainali na Mehalla El Kubra ya Misri kwa mikwaju ya penalti 3-0 jijini Cairo, baada ya kila timu kushinda bao 1-0 nyumbani.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema mechi itakuwa ngumu, lakini watahakikisha wanapigana kufa au kupona kupata matokeo ambayo yatawaweka vizuri kwenye mechi ya marudiano hapa nchini Jumamosi ijayo.

"Tofauti na watu wanavyofikiria kuwa mechi itakuwa rahisi, si hivyo. Tumefuatilia mechi zao na tumeangalia mechi yao walizocheza hivi juzi, ni wachezaji ambao wana nguvu, warefu na wanacheza mpira wa kasi sana. Tumewaambia wachezaji wetu juu ya hilo kuwa jamaa wanakimbia sana, wana nguvu na warefu, hivyo ni wazuri sana kwenye mipira ya juu na faulo pia," alisema Matola.

Hata hivyo, alisema pamoja na uzuri wao, lakini nao wana matatizo upande wa beki.

"Hawa jamaa ni wazuri sana mbele, kwa hiyo tumejipanga kwa hilo, ila si wazuri sana nyuma. Mabeki wao ni wazito, kwa hiyo hilo litakuwa ni faida kwetu na tunaweza kutumia udhaifu wao kupata ushindi au mtokeo ambayo yataweza kuturahisishia kazi," alisema Matola.

Golikipa wa timu hiyo, Aishi Manula, naye alisema mechi itakuwa ngumu, lakini wao wamejipanga kuonyesha watu kuwa Simba haikubahatisha kufika hapo ilipo.

"Jamaa ni wazuri, wana kasi, lakini na sisi tuna wachezaji wazuri pia, tutapambana na mashindano haya makubwa ndiyo ya kuonyesha kuwa sisi pia tunaweza. Sisi kama wachezaji tunataka tufike hatua ya nusu fainali kwanza, mengine yatakuja baadaye na uwezo huo tunao," alisema Manula ambaye amekuwa kwenye kiwango kizuri kwa sasa.

Katika mchezo wa Jumatano wa Ligi Kuu Afrika Kusini kati ya Kaizer Chiefs na Moroka Swallows, ambao ulimalizika kwa sare ya bao 1-1, Gomes alizuiwa kuingia uwanjani kutokana na wapinzani wao hao kuhofia atakisoma kikosi chao, huku maofisa wengine wa benchi la ufundi la Simba wakiruhusiwa.

Simba imefika hatua hiyo baada ya kuongoza kwenye Kundi A lililokuwa likijumuisha mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan huku Kaizer Chiefs ikishika nafasi ya pili kwenye Kundi C lililokuwa na Wydad Casablanca ya Morocco, Horoya FC ya Guinea na Petro de Luanda ya Angola.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002